**Biteko** UK. 3
awa mbogo wanaotafuta uongozi kwa njia ya fedha

**ACT** yataka NFRA ichunguzwe kwa madai kuchelewa malipo wakulima
UKURASA 3

**MAISHA;** Dada wa kazi ni bora kuliko binti yako!
UKURASA 11



UKURASA 9


# Nipashe JUMAPILI
MWANGA WA JAMII
Jumapili Septemba 15, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/
ISSN 0856 • No. 0581800
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




# Utata wagubika kifo cha daktari

• **Mwili** wakutwa porini pembeni kukiwa na dawa, adaiwa kumtumia mke ujumbe... *endelea ukurasa 3*

## "Amri nane' kuwanusuru Watanzania maradhi sugu
UKURASA 2

# Fedha na mifugo vyaelezwa kuchochea ukeketaji watoto
UKURASA 2



Watendaji wa uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura ambao ni Mratibu wa Uandikishaji wa mkoa, Maofisa Waandikishaji na Waandikishaji Wasaidizi ngazi ya jimbo, Maofisa Uchaguzi, Maofisa Ugavi na TEHAMA wa Halmashauri ya mkoa wa Dodoma, wakila kiapo cha kujitoa uanachama na kile cha kutunza siri, kabla ya kuanza mafunzo ya siku mbili, kuhusu uboreshaji, jijini Dodoma, jana. **PICHA: INEC**

**MICHEZO** **YANGA YATANGULIZA MGUU MAKUNDI CAF** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Waibua upya hoja mgombea binafsi

**Na Pilly Kigome**

WADAU wa demokrasia wameibua upya hoja ya mgombea binafsi, wakieleza kuwa itaondoa manyanyaso, udhalilishaji na chuki.

Akizungumza katika maadhimisho Siku ya Demokrasia Duniani yaliyoandaliwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), yaliyofanyika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), mwanasiasa na msomi nguli, Prof. Anna Tibaijuka, alisema iwapo mapendekezo hayo yatafanyiwa kazi, baadhi ya viongozi watarajiwa wanaokutana na manyanyaso ndani ya vyama vyao, watasimama katika uchaguzi.

Prof. Tibaijuka alisema Tanzania imepiga hatua kubwa katika demokrasia angalau kumekuwa na mwamko wa ushirikishwaji wa makundi maalum wakiwamo wanawake, vijana na watu wenye ulemavu Tanzania Bara na Visiwani Zanzibar.

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Dk. Anna Henga, alisema moja ya eneo mtambuka katika haki za demokrasia ni ushiriki wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika vyombo vya uamuzi na michakato ya kiuchaguzi.

Alisema kwa miaka mingi kama taifa kumekuwa hakuna sheria mahsusi zinazoainisha utaratibu utakaohakikisha ushiriki au kuongezeka kwa makundi hayo ukiondoa ule wa viti maalum ulioainishwa katika Ibara ya 66 na ule wa wabunge wa kuteuliwa na Rais kwa mamlaka aliyopewa na Katiba ya Mwaka 1977.

Dk. Henga alisema licha ya kuwapo wa mfumo huo, bado kumekuwapo na malalamiko ya wadau kutokana na mfumo huo kuwa na mapungufu, eneo la vijana na watu wenye ulemavu bado hakuna mfumo wowote wa kisheria unaoainisha ushiriki wa kundi hilo katika vyombo vya maamuzi.

"Nchi yetu inaelekea kwenye matukio makubwa mawili yanayoshabihiana na demokrasia, lile la uandikishwaji na uboreshwaji wa daftari la kudumu la wapigakura na Uchaguzi wa Serikali za Mtaa, hivyo siku hii ni maandalizi kuelekea matukio hayo," alisema.

Balozi wa Norway nchini Tanzania, Tone Tinnes, alisema demokrasia ni mhimili mkubwa kwa binadamu na kuomba asasi za kiraia vyama vya siasa na serikali kuungana kwa pamoja katika kuijenga.

Alisema demokrasia na maendeleo ni vitu vilivyofungamana kwa pamoja na nchi inapokuwa na uhuru wa kujieleza itasonga mbele na kuwa na maendeleo makubwa kwa kuwa nchi zote zilizoendelea hakukuwa na kuminywa kwa uhuru wakujieleza.

Katibu Mkuu wa Baraza la Vijana CHADEMA (BAVICHA), Catherine Magige, alisema katika ajenda ya maendeleo huwezi kumuondoa mwanamke katika jamii, hivyo kumekuwa na changamoto kubwa katika kufanya siasa mtu wa jinsia hiyo hasa katika vyama vya upinzani kutokana na mifumo iliyowekwa katika uchaguzi.

Alisema kuna mambo mengi ambayo yanaogopesha hususani kwa wanawake na Tume ya Uchaguzi imekuwa ikifinya na kufumbia macho baadhi ya vitendo vinavyojitokeza katika uchaguzi huku mfumo mzima wa uchaguzi ukiwa hauko sawa hasa katika kutumia vyombo vya dola vibaya.

# Fedha na mifugo vyaelezwa kichocheo ukeketaji watoto

**Na Shaban Njia,** TARIME

UTOAJI wa zawadi mbalimbali zikiwamo ng'ombe na fedha kwa wazazi wanaowafanyia ukeketaji watoto wao zimetajwa kushawishi na kusababisha ongezeko la vitendo hivyo.

Kutokana na hali hiyo, wananchi wameiomba serikali kushirikiana na wadau kudhibiti matukio hayo ya ukatili wa kijinsia yanayovua utu wa binti.

Ombi hilo walilitoa katika kikao cha kuweka mikakati ya kuzuia ukatili wa kijinsia wilayani Tarime, mkoani Mara kupitia mradi wa "Haki Yangu Chaguo Langu".

Mradi huo unatekelezwa na Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF) kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) kwa ufadhili wa serikali ya Finland.

Mkazi wa Kijiji cha Susuni, Penina Samson, alisema ukeketaji hauwezi kwisha kwa haraka kwa sababu wazazi wenye watoto wanapewa zawadi ya fedha, kanga, vitenge na wakati mwingine mbuzi na ng'ombe kama zawadi za kumfanyia mtoto ukeketaji.

Alisema zawadi hizo hutolewa siku ya sherehe za kuwafanyia ukatili mabinti.

Samson alisema ili kuondoa tatizo hilo ni vema kuwafikia wananchi wa vijijini na kuwaelimisha kuhusu madhara yake na baadaye kuanza kuwachukulia hatua kali za kisheria, wazazi na walezi wanaoshiriki kuendeleza na adhabu zao zitangazwe katika vyombo vya habari.

Bhoke Marwa alisema baadhi yao wamekuwa wakiwafanyia ukeketaji watoto wachanga kwa kurubuniwa na wakwe zao na kliniki ya kwanza wanapowapeleka hospitalini au vituo vya afya, anakuwa tayari ameshakeketwa.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Korotambe, Kata ya Mwema, Joseph Chacha, alisema kumekuwapo na unyanyasaji unaombatana na udhalilishaji wakati wa ukeketaji kwa watoto wa kike, kwa kuvuliwa nguo mbele za watu, kitendo ambacho sio sawa na kinapaswa kukemewa.

Mratibu wa Haki Yangu Chaguo Langu kutoka WiLDAF, Joyce Kessy, alisema uundwaji wa sheria ndogo katika vijiji utasaidia kukabiliana kwa kiasi kikubwa na tatizo hilo.

Alisema bila kuweka sheria zitazowabana, wahusika wa ukeketaji wataendelea bila kificho wakiamini wanatekeleza mila bila kujua hawatendi haki kwa watoto.

Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Meja Edward Gowele, alisema hata sita kuwachukulia hatua za kisheria wale wote watakaobainika kuendeleza vitendo hivyo katika jamii, kwani vinavua utu na udhalilishaji wa binti.



Spika wa Bunge na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), Dk. Tulia Ackson (kushoto), akizungumza jambo na Rais wa Armenia, Vahagn Khachaturyan, baada ya kuhitimishwa kwa Mkutano wa 10 wa Wabunge Vijana wa IPU, jijini Yerevan, nchini humo, jana. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# 'Amri Nane' kunusuru Watanzania magonjwa sugu

**Na Romana Mallya**

KASI magonjwa yasiyoambukiza imewashtua wadau na sasa katika kunusuru taifa kuangamia wamekuja na mambo manane waliyoyabatiza kama 'amri nane' kusaidia watanzania kuwa na mtindo bora wa maisha.

Mwenyekiti wa Chama cha Wagonjwa wa Kisukari Tanzania (TDA) na Mwenyekiti Shirikisho la Vyama vya Magonjwa Yasiyoambukiza Tanzania (TANCDA), Prof. Andrew Swai, aliyataja mambo hayo juzi mkoani Dar es Salaam katika mafunzo waliyoandaa kwa waandishi wa habari kuhusu magonjwa hayo.

Prof. Swai alitaja la kwanza kuwa ni watu wanapaswa kuzingatia kila mlo wanaokula lazima uwe na aina zote za vyakula.

"Tunakula kujenga na kupata joto/nguvu na kinga ya mwili. Aina tano za vyakula ni nafaka, mizizi, ndizi mbichi za kupika, matunda, mbogamboga, jamii ya mikunde na asili ya wanyama na mafuta," alisema.

Mtaalam huyo alitaja la pili kuwa ni watu wasichakachue vyakula wanavyokula kila siku.

"Sukari huharibu meno na tatizo la meno kuoza ni kubwa, wengi meno yameharibika kwa sababu ya ulaji wa sukari kwa wingi, asali nayo ni sukari wakati mwingine huwa tunasahau tukifikiria ni salama hapana, imejaa sukari kweli. Tukumbuke vyakula hubadilishwa kuwa sukari tumboni, si mdomoni.

Alikumbusha kuwa watu wasitumie zaidi ya vijiko vitano vya sukari kwa siku wala kutumia vyakula au vinywaji vilivyoongezwa sukari.

"Oksijeni tunayopumua huunguza sukari mwilini ili tupate joto/nguvu. Jikoni moto ukizidi nyama huungua, mwilini sukari ikizidi mwili huungua," alikumbusha. Prof. Swai alitaja jambo la tatu kuwa ni watu wasile kwa wingi hadi kunenepa, huku akielimisha kwamba vyakula vyote huweza kunenepesha.

Alikumbusha kuwa watu wasizidishe kijiko kimoja cha chumvi kwa siku kwa sababu huongeza msukumo wa damu.

"Tumia mafuta kidogo tu ya mimea si ya wanyama kwa sababu mafuta mengi huchangia kuziba kwa mishipa ya damu. Usizidishe vilevi kwa sababu huchangua kuharibu ubongo, moyo, kongosho na ini na matibabu ni gharama," alisema.

Jambo la nne, alilitaja kuwa ni watu wapende kushughulisha mchana kwa sababu huondoa chumvi mwilini na kufanya mzunguko wa damu usiongezeke, hupunguza unene na msongo wa mawazo, huimarisha misuli/mifupa na kuongeza kinga ya mwili.

Alisisitiza kwamba kila saa mtu anapaswa kushughulisha mwili kwa angalau dakika tano na kutoa jasho kwa angalau dakika 30 kila siku.

"Tano, tupumzike usiku tulale angalau saa saba ili mwili kuweza kujikarabati, sita usitamani vya watu, ukiwa na tamaa mbaya alafu malengo yasipofikiwa huleta msongo wa mawazo na kuna uwezekano wa kupata kisukari, msukumo wa juu wa damu na saratani.

"Saba, epuka tumbaku kama tunavyojua tumbaku huchangia magonjwa mengi na la mwisho chunguza afya kila mwaka," alisema.

Prof. Swai alisema magonjwa mengi yasiyoambukiza hayana dalili hadi mwili umeshadhurika vibaya, hivyo ni lazima watu kujenga tabia ya kuchunguza afya zao angalau mara moja au mbili kwa mwaka ili kujua hali zao.

Msaikolojia Tiba na Mtaalam wa Afya Akili, Isaac Lema, ambaye pia ni kiongozi wa Chama cha Afya Akili Tanzania, alisema afya ya akili nayo hutakiwa kuchunguzwa kama magonjwa mengine.

"Tunapozungumzia afya ya mwili na afya ya akili iwe bora na nzuri. Hata tukizungumzia afya ya akili mahali pa kazi tumegundua watu wengi tulianza kazi tukiwa na afya bora ya akili, hatukuanza na afya duni ya akili.

"Ukiitafuta hiyo afya bora nenda kwenye CV (wasifu) yako ulijiandaa. Afya ya akili inaruhusu mwonekano wako uzungumze na mtu unayekutana naye.

"Pamoja na kwamba kuna afya tukumbuke kuna changamoto ya magonjwa, na magonjwa yanapokuja afya inaweza kubaki bora au ikawa duni.

## HABARI KITAIFA

# ACT yataka uchunguzi NFRA malipo wakulima

**Na Halfan Chusi**

KIONGOZI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Dorothy Semu, amemtaka Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuichunguza Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), ili kujua sababu ya wakulima kucheleweshewa malipo ya fedha zao.

Semu aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wananchi katika mkutano wa hadhara uliofanyika Handeni, mkoani Tanga, ikiwa ni mwendelezo wa ziara ya chama hicho.

Baada ya kupokea malalamiko hayo kutoka kwa baadhi ya wananchi, Semu alisema kwa ukuaji wa teknolojia katika ulimwengu wa sasa, inashangaza kuona zinapita mpaka siku 14 mkulima hajalipwa fedha zake.

Alisema walitegemea NFRA ingemsaidia mkulima apate mahali salama pa kuuza mahindi yake kwa bei nzuri ili afaidike na kilimo chake, lakini badala yake wamepokea taarifa nyingi kutoka kwa wakulima mahindi namna wanavyonyanyaswa.

"Tuna serikali ambayo haisikilizi shida za wananchi, tumesikia Bunge linapitisha bajeti, badala ya kupunguza mzigo wa kodi kwa wananchi limeenda kuongeza, tulikuwa tunalipia kodi ya nyumba Sh. 1,000, sasa hivi ni Sh, 2,000 hiki ni kielelezo tosha kwamba, umeshindwa kumtoa Mtanzania kwenye wimbi la umaskini.

"Ukiangalia maeneo mengi ya vijijini, mambo ni yaleyale hakuna umeme, maji, shule, vituo vya afya. Hapa Tanga wananchi wamejitolea kujenga zahanati, lakini hata kuwawekea umeme imeshindikana," alisema.

Semu alisema Tanga inaongoza kwa kilimo cha mahindi ikizalisha asilimia 65, huku mwaka 2019/20 uzalishaji ulikuwa zaidi ya tani 429.

Akiwa mkoani Mtwara, Katibu Mkuu wa chama hicho, Ado Shaibu, aliwataka wananchi wa Kusini kuwa mstari wa mbele kuwafichua watu wanao wanyonya katika mazao ya ufuta, korosho, na mbaazi ambayo yamekuwa yakilalamikiwa mara kadhaa.

"Msiwe wanyonge, tupeni ushirikiano wa watu wanaowanyonya na kuwadhurumu haki zen. Nipo tayari, acheni uoga, tutawaweka hadharani na hatua zitachukuliwa. Kusini imegeuzwa kama chapati, sekta ya kilimo inachezewa sana," alidai.

Shaibu aliahidi kuendelea kuwatetea na kukataa wizi hadharani na kwamba, yupo tayari kifo chake kitokane na mapambano ya haki.

Alisema takwa lao ni kila atakayeshinda ndio atangazwe sio kiongozi mmoja atoe kauli ya aliyeshindwa ndio atangazwe.

# Utata wagubika kifo cha daktari

**Na Vitus Audax**

UTATA umeibuka kuhusu kifo cha Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Ulyankulu, Kaliua mkoani Tabora, Dk. Dismas Chami, aliyetoweka siku 11 zilizopita baada ya mwili wake kukutwa porini.

Mwili wa daktari huyo umekutwa katika pori huko Kaliua, huku pembeni kukiwa na dawa mbalimbali za hospitalini.

Taarifa zilizosambaa mitandaoni mapema jana, zilieleza kuwa Dk. Chami aliondoka nyumbani kwake Septemba 4, mwaka huu, akimuaga mke wake kuwa angerejea kesho yake.

Hata hivyo, hakurejea na alipotafutwa kupitia simu yake hakupatikana na ilipofika Jumatano ya wiki hii (Septemba 11) ilipatikana lakini kila alipopigiwa hakupokea.

Taarifa hizo zinaeleza kuwa baada ya kutokupokea simu muda mrefu, inadaiwa kwa alituma ujumbe mfupi kwa mke wake uliosomeka hivi, "Nisamehe sana, baada ya dakika chache sitakuwa nanyi duniani, simamia kila kitu nilichokiacha pesa zote zipo CRDB bank, simamia watoto wasome kwaheri."

Inaelezwa kuwa baada ya ujumbe huo, simu yake haikupatikana tena na Jeshi la Polisi lilimtafuta bila mafanikio na ndipo jana mwili wake uliokotwa maeneo ya Malolo ukiwa umechomwa sindano.

Taarifa hizo zinaeleza kuwa pembeni mwa mwili huo kumekutwa na dawa mbalimbali za hospitalini ambazo zinadaiwa kutumika kujidunga au kudungwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Richard Abwao, alipotafutwa na Nipashe ili kuzungumzia tukio hilo simu zake ziliita bila kupokewa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi Mkoa ambaye pia ni Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Paul Chacha, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa mganga huyo hakuuliwa, bali alijiua mwenyewe kwa mujibu wa taarifa za uchunguzi kutoka Jeshi la Polisi.

"Yeye mwenyewe aliacha ujumbe akimtaka mke wake kulinda na kusimamia familia, hivyo tukio hilo halihusiani na kuuliwa.

"Hivyo utaratibu wa vipimo bado unaendelea, lakini ujumbe huo wamemkuta nao mke wake na kuthibitisha hilo.

"Jeshi la Polisi litakuja na taarifa rasmi kuhusu ni nani? Amekutwa wapi? Na vipimo vya kitabibu vinasema nini? Kuhusu kilichomkuta yote hayo yakiwa tayari umma utajulishwa baada ya madaktari kufanya postmortem (uchunguzi wa maiti).

Kuhusu madai ya kuwapo kwa mgogoro wa kifamilia kupitia taarifa za familia yake, Chacha alisema kuwa hakuna mgogoro wowote, kwani ujumbe ulioachwa haukuonesha.

Mkuu wa Mkoa huyo alisisitiza kwamba suala hilo linaendelea kuchunguzwa na hadi kufikia leo (Jumapili) majibu yatakuwa yamepatikana.

"Ieleweke kuwa hii ni taarifa ya mwanzo, kwani polisi na madaktari bado wanaendelea na uchunguzi, hivyo kama kutakuwa na taarifa kamili tutazitoa na kuueleza umma, ili kuondoa taarifa za upotoshaji zinazoendelea," alisema Chacha.



Kiongozi mstaafu wa Chama cha ACT Wazalendo, Zitto Kabwe akihutubia mkutano wa hadhara wa chama hicho, katika Kata ya Ruhuhu, Jimbo la Ludewa, mkoani Njombe, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Biteko aonya watu kusaka uongozi kwa fedha

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, ameonya watu wanaotumia fedha kusaka uongozi wakati wa uchaguzi.

Amesema katika kuelekea kipindi cha uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba, mwaka huu, na Uchaguzi Mkuu utakaofanyika mwakani, mtu kuwa na fedha isiwe sehemu ya sifa ya kupata uongozi.

Alisema hayo jana wakati akifunga maonesho ya saba ya kitaifa ya Mifuko ya Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi yaliyokuwa yakifanyika mkoani Singida kuanzia Septemba 8 hadi 14, mwaka huuu.

Biteko ambaye alimwakilisha Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema akitokea mtu ambaye hana fedha na hali yake ni ngumu kimaisha lakini ana mawazo mazuri ya kuwaongoza wananchi kwenye mitaa,kitongozi au kijiji wananchi wamchagule.

"Sifa ya kuchagua kwa sababu ya mtu mwenye fedha naomba isiwe sehemu ya kwenye uchaguzi huu,tuchaguane kwa sifa,tusichaguane sababu ya ukabila huyu ni Mnyaturu mwenzangu au Mnyiramba mwenzangu,tuchaguane kwa sababu ya uwezo," alisema.

Alisema wananchi wasifanye kosa kuchagua viongozi ambao hawana uchungu na maendeleo yao na taifa kwa ujumla.

Dk. Biteko alisema uchaguzi wa serikali za mitaa si uchaguzi mdogo ni mkubwa kwa maendeleo ya nchi hivyo wachaguliwe viongozi wanaojua shida za watu.

"Wewe uliyesoma au wewe mwenye takriba ya juu sasa usione uchaguzi huu haukuhusu ni uchaguzi muhimu wa kutafuta viongozi wanaojua shida za watu kuanzia Januari hadi Desemba, kuanzia Jumatatu hadi Jumapili na kuanzia saa moja asubuhi hadi saa moja jioni," alisema.

Aliongeza kuwa ili serikali iwawezeshe wananchi kiuchumi lazima kuwe na viongozi ambao wana uchungu na maendeleo ya watu ambao wakiamka wanawaza tu maendeleo.

"Wako madiwani wanahitaji viongozi wa serikali za mitaa wazuri ambao watabeba shida za wananchi zinazowakabili. Mkichagua viongozi kwa kuangalia kwamba tunaabudu pamoja au ana uwezo wa kifesha, mtakuwa hamwatendei haki watoto wa watoto wenu ambao watakuwa wanaamini sifa bza kifedha,ukabila na udini zimewapa nafasi ya kuwa viongozi," alisema.

Biteko alisema mwaka huu Mifuko ua Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi imepiga hatua kubwa kiuchumi kwa kuwafikia watanzania wengi zaidi na kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, alisema zaidi ya Sh. bilioni 2.5 ziko benki na zitatumika kutoa mikopo kwa wanawake, vijana na makundi maalum kwenye halmashauri za wilaya za mkoa wa singida.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Uwezeshaji Wananchi, Being' Issa, alisema maonesho hayo mwakani yatafanyika mkoani Mwanza.

# Mavunde awapa mchongo watoa huduma migodoni

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Madini, Anthony Mavunde, amewataka Watanzania wanaoshiriki katika mnyororo wa thamani wa sekta ya madini kuchangamkia fursa kubwa iliyoko ya ununuzi wa bidhaa na utoaji huduma migodini.

Amesema kwa mwaka wa fedha 2023/24, jumla ya Sh. trilioni 3.1 zimetumika katika eneo la ununuzi wa bidhaa na huduma.

Mavunde aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa hafla ya uzinduzi wa Chama cha Watoa Huduma na Wasambazaji wa Bidhaa Migodini (TAMISA).

Alisema uwekezaji nchini Tanzania katika sekta ya madini unakua siku hadi siku na hiyo inatokana na mazingira mazuri ya uwekezaji yaliyowekwa na serikali.

Alisema chama hicho kitasaidia kuwa na sauti ya pamoja katika kuwajengea uwezo Watanzania na kuwaimarisha ili kuwa shindani katika utoaji wa huduma na usambazaji wa bidhaa migodini.

"Ninatamani sana kuziona hizi Sh. trilioni 3.1 zinabaki mikononi mwa Watanzania ili kuchochea uchumi wa nchi yetu kwa kuanzisha viwanda vya kuzalisha bidhaa na huduma zenye mahitaji makubwa migodini," alisema.

Waziri Mavunde alipongeza TAMISA kwa kupokea na kuyafanyia kazi maagizo yake ya uanzishwaji wa chama cha watoa huduma na wasambazaji wa bidhaa migodini, huku akiwaeleza kuwa anaamini watakuwa jukwaa zuri la mafanikio ya sekta binafsi Tanzania.

Mwenyekiti wa TAMISA, Peter Kumalilwa, alisema chama hicho kina malengo mahsusi ya kuwaleta pamoja watoa huduma na wasambazaji wa bidhaa migodini, kuishauri serikali namna bora ya kuwajengea uwezo watanzania kunufaika na sekta ya madini na kushirikiana na serikali kutatua matatizo ya msingi katika suala la Local content (maudhui ya ndani).

Akitoa salamu za sekta binafsi, Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPS) na Mwenyekiti wa Kongani ya Huduma, Octavian Mshiu, alipongeza hatua ambazo serikali inazichukua kwa sasa kuvutia uwekezaji na kukuza sekta binafsi nchini.

Aliahidi kuwa TPSF itakuwa bega kwa bega na wadau wote kuhakikisha watanzania wanachangamkia uchumi wa madini.



Waziri wa Afya, Jenista Mhagama (wa tatu kulia), akipokea msaada wa magari maalumu yenye huduma ya upasuaji kutoka kwa Mwakilishi wa kampuni ya Sotac ya nchini Uholanzi, Suzanne Holtz, kwa ajili ya Hospitali ya Benjamini Mkapa jijini Dodoma, jana. Wengine ni Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Laizer Saitori (kulia) na (wa pili kulia) Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Prof. Abel Makubi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wataka mkazo elimu usajili biashara

**Na Vitus Audax,** MWANZA

BAADHI ya wafanyabiashara kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa, wameiomba serikali kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) kuongeza mkazo katika kutoa elimu ya usajili biashara na kampuni ili kurasimisha biashara zao.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti kuelekea kilele cha Manesho ya Biashara ya Afrika Mashariki yanayoendelea jijini Mwanza, wafanyabiashara hao wamesema licha ya huduma hiyo kuwa muhimu baadhi yao wamekuwa hawaipati kwa wakati.

Mmoja wa wafanyabiashara hao ,Seraphini Kimaro, mmiliki wa kampuni, alisema kwa wafanyabiashara kuna mambo mengi wamekuwa hawajui kutokana na elimu kutokuwafikia, hivyo kuomba serikali kuweka jitihada katika kuwafikia.

"Kama leo nimepata fursa ya kuhuisha taarifa zangu lakini huduma hii nimeikosa kwa muda mrefu, hivyo tunaomba hata ikifanyika kila baada ya kipindi fulani lengo liwe ni kuwafikia wafanyabiashara na wamiliki wa kampuni kwa uharaka," alisema Kimaro.

Salome Nsumba alisema awali hakuwa na elimu juu ya umuhimu wa usajili wa biashara zake hali iliyosababishwa na kutokuwa na elimu ya kutosha na kuendelea na shughuli zake bila kutambulika kisheria.

"Nilipofika kwenye maonesho haya nimebaini kuwa suala hili ni muhimu na ni vyema litiliwe mkazo ili wafanyabiashara na wamiliki wa kampuni wengi wajisajili na kujua umuhimu wake kitaifa na kimataifa.

Kuhusu juhudi zoinazofanywa na BRELA kuhakikisha wanawafikia wafanyabiashara ili kujisajili na kusajili majina ya biashara, Ofisa Sheria wa Wakala, George Msaki, alisema wamekuwa wakipita katika vyuo vikuu, mitaani na maonesho mbalimbali ili kuhakikisha huduma hiyo inawafikia.

"Lakini pia kwa sasa huduma zetu zinapatikana kupitia mfumo wa kiditali unaoitwa 'online registration system (ORS) ambao ni rafiki unafikiwa kwa njia ya simu za mkononi kwa simu janja na komputa," alisema.

Pia alisema mfumo huo unarahisisha utolewaji huduma hiyo kwa kuhitaji taarifa kidogo na kuwa mtu yeyote anaweza kuutumia bila kufika ofisini kupitia tovuti ya wakala au msaada kupitia namba za simu zinazotolewa katika tovuti hiyo.

Naye Ofisa Leseni wa BRELA, Sweetness Madata, alisema kwa mtu yeyote ambaye anafanya bisahara yoyote ya Leseni 'A' kama hajatii matakwa ya leseni yake kwa kusajili, anakwenda kinyume cha sheria.

Aliwataka wafanyabiashara wote kutimiza takwa hilo la kibiashara ili kufanyabiashara zao kwa kujiamini ikiwa ni pamoja na kuaminiwa kimataifa na wateja wao wote wanaofanya nao biashara.

# Mhagama azindua huduma saba BMH

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Jenista Mhagama, amezindua huduma saba katika Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) vikiwamo vyumba vya upasuaji vinavyotembea ambavyo vitaendelea kuimarisha huduma za afya kwa jamii nchini.

Huduma nyingine ni pamoja na kutengeneza miguu bandia, miongozo ya matibabu, kitengo cha huduma kwa wateja, maabara maalum, vyumba vipya vya upasuaji, miongozo ya idara ya kutoa huduma.

Akizungumza juzi katika uzinduzi huo, Mhagama aliagiza zitumike ipasavyo kwa jamii, huku akiwapongeza watumishi hospitalini huko kwa ubora wa huduma za afya wanazotoa.

"Ninampongeza Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali, Prof. Abel Makubi, na timu nzima ya watumishi wenzake kwa huduma nzuri na ufanisi katika kuboresha huduma za afya," alisema.

Waziri Mhagama alisema BMH ni hospitali kubwa, hivyo inapaswa kuendelea kujitangaza kwa kutoa huduma bora ndani na nje ya nchi.

Kila huduma aliyoizindua, alisema ina kazi maalum, na kuagiza watumishi kuzitumia vizuri ili uwekezaji wa serikali kwenye sekta ya afya ufanyike.

Alisema serikali inahitaji kuona huduma za afya zinatolewa kwa jamii ipasavyo kutokana na uwekezaji unaofanywa.

Prof. Makubi alisema watumishi hospitalini hapo wameshirikishwa katika kuandaa Standard Operating Procedures (SPO) 'Taratibu za Kawaida za Uendeshaji'

"Ninawasifu sana watumishi wangu wa BMH wameshiriki kikamilifu katika kuandaa SPO ambazo zitatuongoza katika kutoa huduma," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya BMH, Dk. Deodatus Mtasiwa, alisema uanzishwaji wa hospitali hiyo umetokana na muhtasari wa hospitali kama saba za India.

"Hata mchoraji wa Hospitali hii ni mtanzania baada ya kuangalia muhtasari wa hospitali saba za India," alisema Dk. Mtasiwa.

# MATUKIO KATIKA PICHA



Mafundi wa mkandarasi wakitengeneza miundombinu ya maji ya mvua katika ujenzi unaoendelea wa barabara ya m basi yaendayo haraka katika Mtaa wa Azikiwe, katikati ya Jiji la Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**




Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi na Biashara za Kati wa Benki ya Exim, Andrew Lyimo (wapili kushoto), akizungumza wakati wa droo ya mwisho ya kampeni ya Tap Tap Utoboe, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, iliyokuwa na lengo la kuhamasisha wateja wake, kufanya miamala kutumia simu za mkononi na mtandao. Wengine ni Mkaguzi na Mdhibiti kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania, Lucy Katamba (kushoto) na Mkuu wa Idara ya Masoko na Mawasiliano wa benki hiyo, Stanley Kafu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Shekhe wa Mkoa wa Dar es Salaam, Omary Kawambwa (wa nne kushoto mstari wa mbele), akiwa katika picha ya pamoja na wadau mbalimbali baada ya kukabidhi vifaa maalum vyenye thamani ya Sh Milioni 3, katika Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, kwa ajili ya matumizi ya wagonjwa hospitalini hapo. **PICHA: ASHRACK MIRAJI**



Katibu Tawala Wilaya ya Serengeti, mkoani Mara, Anjelina Marko (wa tatu kulia), akikabidhi moja ya vyerahani vilivyotolewa msaada na Chuo cha World Changer Vision Tanzania, kwa wahitimu wa fani ya ushonaji wa chuo hicho, mjini Mugumu, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Mchuuzi wa nyama choma akitumia toroli kama nyenzo inayomrahisishia kutembeza biashara yake ya mishikaki na ndizi, kama alivyonaswa na kamera yetu, katika eneo la Makumbusho, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: SABATO KASIKA**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mivutano hii haina tija katika ustawi wa amani

**"WAPIGANAPO** tembo ni nyasi ndizo ziumiazo" msemo huu umezoeleka miongoni mwa watu ndani na nje ya Tanzania kuonesha kuwa misuguano baina ya wanyama hao ina athari kubwa kwa rasilimali hiyo ambayo Mwenyezi Mungu aliumba ili mwanadamu na viumbe vingine waifurahie.

Pamoja na kwamba imezoeleka hivyo, mwasisi wa taifa la India, Mahatma Gandhi, aliwahi kusema si tu Wanyama hao wapiganapo bali pia hata wanapofanya mapenzi. Hiyo ni kutokana na ukubwa wao kwa sababu matendo yao yoyote, yawe ya amani au shari, yana athari kubwa kwa viumbe hai vingine.

Misemo hiyo inasadifu na hali ya sasa nchini kutokana na mivutano inayoendelea kati ya Jeshi la Polisi na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA). Katika mvutano huo, Jeshi la Polisi limekionya chama hicho kuhusu azma yake ya kuandamana ifikapo Septemba 23, mwaka huu, kwa kile kinachoeleza kuwa ni hatua inayotokana na chombo hicho chenye dhamana ya kulinda usalama wa raia na mali zao.

Chanzo hasa cha mpango huo wa CHADEMA kuandamana ni madai ya jeshi hilo kushindwa kuchukua hatua dhidi ya matukio ya utekaji na mauaji ya wanachama wao wakiwamo viongozi waandamizi.

Jambo hilo limekuwa kubwa zaidi baada ya Mjumbe wa Sekretarieti ya CHADEMA na Msaidizi wa Katibu Mkuu wa chama, Ali Kibao, aliyetekwa hivi karibuni na watu wanaodaiwa kuwa polisi wakiwa na bunduki, akiwa kwenye basi akienda Tanga na baadaye mwili wake kukutwa eneo la Ununio, Dar es Salaam ukiwa umeharibiwa vibaya kiasi cha kushindwa kutambulika.

CHADEMA kwa muda sasa imekuwa ikidai kuwa baadhi ya viongozi na wanachama wake wamekuwa wakitekwa na wengine mpaka sasa hawajulikami kama wako hai au wamekufa. Kutokana na hali hiyo, CHADEMA imetoa muda hadi tarehe hiyo kwa jeshi la Polisi kuweka bayana waliko wanachama na viongozi hao vinginevyo watachukua hatua ya kuandamana.

Kutokana na kauli na kusudio hilo la CHADEMA, Jeshi la Polisi kupitia msemaji wake, Naibu Kamishna (DCP) David Misime, limetoa tamko na kupiga marufuku maandamano hayo huku likionya kuwa mtu yeyote atakayeandamana atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria. Tamko hilo la Misime limesababisha CHADEMA kuibuka na kusema azma yao ya kuandamana iko pale pale.

Kwa ujumla, mivutano hiyo kati ya polisi na CHADEMA haileti afya kwa ustawi wa amani, umoja, upendo na mshikamano pamoja na ustawi wa demokrasia nchini bali inaashiria uvunjifu wa amani na kugharimu maisha ya Watanzania.

Rais Samia Suluhu Hassan, baada ya kutekwa na hatimaye mwili wa Kibao kupatikana, alitoa kauli na kuagiza uchunguzi wa kina ufanyike na apewe majibu haraka. Kauli hiyo imewaamsha baadhi ya viongozi wa CHADEMA na wadau kwamba jambo hilo ni gumu kwa sababu wanaopewa kazi ya kuchunguza wanadaiwa kuwa ni wahusika wa matukio hayo, likiwamo lile la Kibao.

Aidha, Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, alizungumza na wahariri na waandishi wa vyombo vya Habari akieleza msimamo wa chama chake kwamba wanaunga mkono kufanyika kwa uchunguzi huo.

Tangu aingie madarakani, Rais Samia amekuwa akisisitiza umuhimu wa Watanzania, vikiwamo vyama vya siasa, kumaliza tofauti zozote kwa njia ya mazungumzo kupitia falsafa yake ya 4R. Jambo la utekaji wa watu na wengine kukutwa wamepoteza maisha halileti taswira nzuri kwa Tanzania, hivyo halina budi kumalizwa na wadau wote bila kujali imani na itikadi zao.

Kwa mantiki hiyo, ni vyema kama kuna dukuduku lolote kuhusu agizo la kuchunguzwa kwa utekaji na mauaji hayo, kuna umuhimu wa watu kukaa meza moja na kuzungumza njia ipi nzuri. Badala ya kulumbana au kutunishiana misuli.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Hii inaweza kusaidia vita dhidi ya rushwa kwa kizazi kijacho

Na Sabato Kasika

**RUSHWA** ni adui wa haki, utu na heshima ya binadamu, vilevile vitendo vya utoaji na upokeaji rushwa, vimekuwa vikileta vilio karibu sekta zote, sehemu ya kazi na maeneo mengine ya kutolea huduma za kijamii.

Vitendo vya rushwa, kwa namna moja au nyingine, vinakwamisha shughuli za maendeleo kwa mtu mmoja na jamii kwa ujumla, hivyo ni wazi rushwa ni adui wa haki, utu na heshima ya binadamu.

Kila mwaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) anapofanya ukaguzi na kutoa taarifa kwa umma, upigaji mwingi wa fedha za umma umekuwa ukidhihirika, katika taasisi za umma.

Nimaamini kushamiri kwa rushwa, kuna chimbuko lake ambalo ni mmomonyoko wa maadili unaoanzia ngazi ya familia hadi taifa. Hivyo, vita yake ingefikishwa shuleni, wanafunzi wafundishwe somo la maadili.

Mmomonyoko ndio unaozaa maovu, ikiwamo kuenea kwa tatizo hilo, katika maeneo mbalimbali na kusababisha jamii kukosa haki, huku baadhi ya watoaji na wapokeaji wakichukulia kama jambo la kawaida.

Wakati jitihada za kupambana nayo zikiendelea, ninadhani sasa ni wakati mwafaka wa kuwa na mitaala kwa ajili ya somo la maadili, ambalo linaweza kusaidia wanafunzi kuitambua rushwa wangali wadogo.

Serikali imepeleka muswada wa sheria ya rushwa na kutaka adhabu ya faini isiyopungua Sh. milioni mbili na isiyozidi Sh. milioni 10 au kifungo kisichopungua miaka mitano kwa watoaji na wapokeaji wa rushwa.

Hatua hiyo ni nzuri, lakini pia ninadhani kwamba, kupitia somo la rushwa, wanafunzi wanaweza kujua rushwa ni nini, ikiwamo ya ngono, fedha na vitu vingine badala ya kuisikia tu bila kujua maana yake na madhara yake na kujikuta wakijiingiza humo.

**Wakati jitihada za kupambana nayo zikiendelea, ninadhani sasa ni wakati mwafaka wa kuwa na mitaala kwa ajili ya somo la maadili, ambalo linaweza kusaidia wanafunzi kuitambua rushwa wangali wadogo.**

Wanafunzi wakipata elimu kuhusu rushwa na madhara yake, watakapokuwa watu wazima wataendelea kuichukia, kwani watakuwa wameshajua madhara yake tangu wakiwa shuleni.

Hivyo, si vibaya ukawekwa mkakati wa kuanzisha somo hilo kwa shule za msingi hadi juu ili wanafunzi wapate elimu kuhusu rushwa, kwani ni miongoni mwa mambo ambayo yanachangia mmomonyoko wa maadili.

Ninaunga mkono juhudi mbalimbali ambazo zimekuwa zikifanywa za kupambana na rushwa, ikiwamo za kuanzisha klabu za wapinga rushwa shuleni, ili wanafunzi wapate elimu ya madhara ya tatizo hilo mapema.

Hatua hiyo ni nzuri kwa sababu inaweza kuaandaaa wanafunzi kupinga rushwa wangali wadogo hata pale wanapokuwa watu wazima wanaendelea kupamba nayo kwa manufaa yao na ya taifa kwa ujumla.

Wakati vita hii ikiendelea, suala la kuwa na somo la maadili ninadhani ni la muhimu, kwani linaweza kusaidia wanafunzi kutambua mambo mbalimbali yanayohusiana na maadili mema.

Kama nilivyoeleza awali, taarifa za kila mwaka za CAG, zimekuwa zikionyesha upigaji mwingi wa fedha za umma, hivyo ni muhimu kuwapo mikakati mbalimbali ya kuwaandaa vyema wanafunzi ikiwamo kupitia somo la maadili. ambalo ninaamini lina manufaa makubwa.

Kwa kawaida, viongozi na watumishi bora wa umma, huandaliwa tangu mwanzo, hivyo kuanzisha somo la maadili shuleni linaweza kusaidia pia kuandaa viongozi watakaoleta manadiliko chanya ya maendeleo ya nchi.

Utaratibu wa utoaji wa elimu kuhusu madhara ya rushwa kutolewa kuanzia shule za msingi, ni mtazamo unaolenga kuhakikisha rushwa inaondolewa nchini kuanzia sasa na hata baadaye.

MAKALA

FIKRA MBADALA

# Watanzania wakiyajua haya, watajua haki zao na kuzidai



Pascal Mayalla

NIANZE kwa kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa 4R na mahubiri yake mazuri kuhusu haki. Tunawaomba watendaji waitafsiri kwa vitendo falsafa hiyo ya 4R kwa kutenda kinachohubiriwa. Yasibaki kuwa maneno lakini vitendo ni tofauti.

Hakuna shaka kabisa kuhusu nia ya dhati ya Rais Samia kutaka Watanzania kutendewa haki. Ana nia njema na thabiti kutaka Watanzania wapate haki zao lakini baadhi ya watendaji wake ndio wanamwangusha.

Haki haileтwi kwenye kisahani cha chai bali ni stahili na stahiki inayopaswa kutolewa bila kuiomba na ikitokea haki haikutolewa au haikutendeka, haiombwi bali inapaswa kudaiwa. Sasa mtu ukiwa hujui haki yako, huwezi kudai kitu usichokijua.

Nikimwangalia na kusikiliza kauli zake kuhusu haki, kusema la ukweli kabisa Rais Samia ana nia njema ya dhati kutoka moyoni mwake kuhakikisha Watanzania wanatendewa haki. Haya mambo ya ajabu ajabu yanayotokea ni uzembe na udhaifu wa baadhi ya watendaji wake. Tunamshauri Rais Samia awe mkali kama Nyerere kwenye ukiukwaji wa haki. Katika hilo ahakikishe hakuna Mswalie Mtume.

Nimekumbushia haki kutokana na kilichotokea hadi kifo cha huyu Mzee Ali Kibao wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA). Kada huyu na mjumbe wa sekretasrieti ya CHADEMA , ameuawa kwa sababu wananchi hawajui haki zao. Kama Watanzania wangekuwa wanajua haki zao Mzee Kibao asingekubali kukamatwa na watu ambao hawatambuliki.

Kwa maana hiyo kama Watanzania wangekuwa wanajua haki zao, dereva wa basi la Tashrif asingekubali kusimamishwa na watu wasiotambulika. Pia dereva wa Tashrif angekuwa anajua ile tiketi ya abiria, ni mkataba wa kisheria wa kumshusha abiria wake kituo alicholipia, dereva ana wajibu wa kisheria, haki ya ulinzi, kuhakikisha usalama wa abiria wake na mali zake kwenye buti la gari yake.

Mali pekee ambayo ni wajibu wa abiria ni mzigo wake mkononi anaoingia nao ndani ya basi, ndiyo "abiria chunga mzigo wako". Jukumu la abiria kufika salama anakokwenda, dereva wa basi ana wajibu wa kisheria kumfikisha huko.

> **Hakuna shaka kabisa kuhusu nia ya dhati ya Rais Samia kutaka Watanzania kutendewa haki. Ana nia njema na thabiti kutaka Watanzania wapate haki zao lakini baadhi ya watendaji wake ndio wanamwangusha.**

Watanzania wangekuwa wanajua haki zao, abiria tu wa kawaida, akiwamo aliyekaa siti namba moja ya basi hilo, ambaye ni askari wa usalama barabarani, alikuwa na uwezo wa kuwabaini majambazi hao kuwa si askari polisi wa kweli na kuwahamasisha abiria wengine wote wasikubali abiria mwenzao atekwe.

Aidha, Watanzania wangezijua haki zao, wangejua polisi haruhusiwi kumkamata mtu yeyote bila kwanza kujitambulisha yeye ni nani na ametokea kituo gani kwa kuonesha kitambulisho cha polisi.

Kadhalika, Watanzania wangejua haki zao, wangejua mtu anayekamatwa ana haki ya kusoma namba ya kitambulisho na kuihakiki namba ya askari polisi kwenye mfuko wa kushoto wa nguo ya polisi. Wakija polisi ambao ni askari kanzu, hawa hawana sare, hivyo hawavai namba. Hawaruhusiwi kumkamata mtuhumiwa bila kuandamana na polisi wenye sare.

Mtu yeyote kabla hajakamatwa, mkamataji lazima awe na waranti au kibali cha kumkamata (arrest warrant) na lazima aripoti ofisi ya serikali ya mtaa husika. Aoneshe 'arrest warrant' atasindikizwa na mtendaji wa mtaa kuja kukukamata.

Baada ya polisi kujitambulisha kwa kuonesha kitambulisho, kitu cha pili ni kuonyesha 'arrest warrant' ili kukwambia unakamatwa kwa kutuhumiwa kwa kosa gani?

Polisi kabla hajamkama mtu anatakiwa kumweza haki zake ikiwamo haki ya kunyamaza kimya, chochote utakachosema kinaweza kutumiwa kama ushahidi mahakamani, na haki ya kuwakilishwa na mwanasheria. Baada yah apo polisi hao watawaeleza hao mashuhuda wanakupeleka kituo gani ili ndugu zako wakufuatilie.

Mtuhumiwa ukifikishwa kituoni kabla hujaandikishwa maelezo, unaaelezwa haki zako ikiwamo haki ya kuwakilishwa kisheria (legal representation).

Haki hizi zikifundishwa kwa wananchi, 'watu wasiojulikana' watapungua na watabaki tu wale wa 'pyu pyu' kama wa Tundu Lissu.

Sote tunajua kwa kauli na matendo, Rais Samia ana nia thabiti na ya dhati watu wapate haki zao na amekuwa akilihubiri hili kwa maneno na vitendo na kuanzisha vitendo, kikosi kazi, tume ya haki jinai.

Kwenye kikosi kazi, Watanzania walitaka tufanye mabadiliko madogo ya katiba ili haki zilizoporwa kinyume cha Katiba zirudishwe. Hili Rais Samia hajalitendea haki lakini abebadili sheria ya uchaguzi na tume ya uchaguzi.

Watanzania wametaka Tume Huru na Shirikishi ya Uchaguzi. Rais Samia ameibadilisha jina kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NECO na kuiita jina jipya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) lakini tume bado ni ile ile!.

Watanzania hawakuomba jina la tume bali ibadilishwe iwe ni Tume Huru na Shirikishi ya Uchaguzi na si kubadilishwa jina lakini tume bado ni ile ile, watu bado wale wale na uchaguzi utaendelea kusimamiwa na makada kindakindaki wa chama kimoja kwenye kofia za wakurungezi wa halmashauri.

Watanzania walitaka sheria mpya ya uchaguzi yenye kutoa haki sawa kwa wote na uwanja sawa wa uchaguzi kwa sababu sheria ikiyokuwapo ilikuwa batili inayokwenda kinyume cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tumeletewa sheria mpya ya uchaguzi yenye ubatili ule ule uliobatilishwa na Mahakama Kuu ya Tanzania kwa kwenda kinyume cha Katiba.

Rais Samia, Watanzania tunakupenda, tunakukubali, tunakuomba mahubiri yako ya falsafa yako ya 4R yasiwe mahubiri tu. Naomba wasisitize watendaji wako watekeleze kwa vitendo.

**Mungu Akubariki uyaweze yote katika Yeye**
**Mungu Ibariki Tanzania**
**Paskali**
**+255 754 270403**

# Naibu Waziri awafunda wanajopo wa kada ya afya, asisitiza uadilifu

**Na Lusungu Helela,** ARUSHA

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deus Sangu, amewataka wanajopo la usaili kuwa waadilifu na kutenda haki huku akisititiza ajira ni suala la usalama wa nchi.

Sangu alitoa kauli hiyo juzi jijini hapa wakati akizungumza na wataalamu kutoka kwenye taasisi mbalimbali za serikali ambao wamechaguliwa kuwa wanajopo wa kuendesha usaili wa mahojiano ya ana kwa ana kwa wasailiwa wa kada ya afya unaendelea katika mikoa mbalimbali nchini.

Alisema serikali imejipanga kuhakikisha haki inatendeka kwa kila msailiwa ili atakayeshinda ashinde kwa haki na atakayeshindwa ashindwe kwa haki.

Sangu alitumia fursa hiyo kutoa rai kwa wanajopo hao kutanguliza mbele maslahi ya taifa huku akionya yeyote atakayethubutu kuvuruga zoezi hilo atakuwa ameingia kwenye matatizo makubwa

"Tunatafuta vijana watakaoingia serikalini katika utumishi wa umma si chini ya miaka 25 na wengine wenye umri mdogo mpaka miaka 30. Kwa hiyo tukifanya makosa tukapeleka vijana wasio na sifa, uadilifu na mengineyo, hivyo tutalighalimu taifa kwa zaidi ya miaka 25," alisema.

Kutokana na hali hiyo, Sangu aliwataka wasaili hao kujiepusha na tabia ya kupendelea na pale inapotea jambo la kujadiliana, wajikite katika kutenda haki.

"Tunataka haki itendeke na ionekane imetendeka kwa wasailiwa wote " alisisitiza Sangu.

Alisema kwa mujibu wa Sera ya Ajira Toleo la Pili la mwaka 2008, inaelekezwa kuwa ajira zote zipatikane kwa ushindani .

"Maombi yamekuwa mengi sana kati ya nafasi 12,000 zilizotangazwa za kada ya afya, zaidi ya vijana 47,000 wameomba huku kwenye walimu vijana walioomba ni 200,000 kati nafasi za ajira za ualimu 11,015 zilizotangazwa, hivyo hakuna njia nyingine ya kupata watumishi pasipo kushindanisha," alibainiosha.

Alisema kwa sasa vijana wengi wamemaliza vyuo na wako mtaani lakini kutokana na bajeti na hali ya Uchumi, serikali haiwezi kuwa na bajeti ya kuajiri vijana wote waliomaliza vyuo

Hata hivyo, alisema serikali imekuwa ikifanya jitihada kubwa na katika kipindi chake cha miaka mitatu, ametoa vibali vya zaidi ya ajira 100,000 ambayo ni idadi kubwa katika kipindi hicho kulinganisha na miaka mitano iliyopita

Naye Kaimu Katibu wa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Mhandisi Samuel Tanguye, alisema usaili huo umeshirikisha watalaamu mbalimbali lengo likiwa kuhakikisha vijana watakaopatika katika machakato huo ni wenye weledi watakaolisaidia taifa

# 11 jela miezi sita kwa kuingia nchini bila kibali

**Na Halima Ikunji,** TABORA

WAHAMIAJI haramu 11 kutoka nchini Burundi wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Wilaya ya Tabora kwa kosa la kuingia nchini bila ya kuwa na kibali na kuhukumiwa kwenda jela miezi sita.

Awali, akisoma hati ya mashitaka Wakili wa Serikali ,Upendo Frolian, alidai mahakamani huko kuwa washtakiwa hao ni raia kutoka Burundi waliingia nchini bila ya kuwa na kibali chochote.

Washitakiwa hao ni Leonard Ndovegwa, Sinzingayo Simon, Issaka Silvery, Ndagishimana Etien, Alex Sado, Nzoiliki Yobu, Fedrick Patrick, Nizikimana Hilali, Nyiyongele Levelie Mbigilimana Sylvesta na Nyongabo Jamali.

Wakili kutoka Ofisi ya Uhamiaji, Allan Sayi l, alidai kuwa washitakiwa hao walikamatwa katika stendi kuu ya mabasi yaendayo mikoani wakiwa wanaelekea Mbeya na wengine wilayani Kaliua wakielekea katika mashamba ya Tumbaku.

Sayi aliiomba mahakama itoe adhabu kali ili iwe fundisho kwa wengine wenye dhamira kama hiyo la kuingia nchini bila ya kuwa na vibali.

Washitakiwa wote 11 baada ya kusomewa shtaka hilo, walikiri kutenda kosa hivyo kuhukumiwa kwenda jela miezi sita.

Baada ya kusikiliza pande zote mbili, Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Wilaya ya Tabora, Sigwa Mzige, aliwatia hatiani washtakiwa hao kutokana kuingia nchini isivyo halili na kuwahukumu kwenda jela miezi sita.

Hata hivyo, alisema watuhumiwa hao wanaweza kulipa faini ya Sh. 500,000 kila mmoja kama mbadala wa adha ya kwenda jela huku akiwaeleza kuwa haki ya rufani iko wazi kwa mshitakiwa ambae hakuridhika na uhamuzi huo.

Washitakiwa wote walipelekwa jela kuanza kutumikia kifungo chao baada ya kushindwa kulipa faini hiyo iliyotolewa na mahakama ili kuwaweka huru.

# Tamasha la utamaduni Ruvuma na fursa kedekede za kiuchumi

Na Mwandishi Wetu

UTAMADUNI ni kielelezo cha jamii na taifa lolote duniani. Bila utamaduni hakuna taifa lililo hai. Utamaduni ndio hutofautisha jamii moja na nyingine na taifa moja na lingine.

Kutokana na ukweli huo, nchini Tanzania makabila mbalimbali na mikoa huandaa matamasha ya utamaduni wa makabila kulingana na jiografia za mikoa ambayo makabila yanayohusika yanatoka.

Ruvuma ni moja ya mikoa ambayo hufanya tamasha kila mwaka na safari hii ni la tatu kitaifa kufanyika mkoani humo. Shamrashamra za tamasha hilo zinaendelea kupamba moto huku Rais Samia Suluhu Hassan akitarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye ufunguzi utakaofanyika Septemba 20, mwaka huu na kutamatika Septemba 23. Makabila mbalimbali yataonesha utamaduni wao.

Wakazi wa mkoa huo wameonesha shauku kubwa ya kushiriki tamasha hilo ambalo wanalielezea kuwa litakuwa la aina yake kwa kuwa pamoja na mambo mengine mbali na faida zingine litasaidia kuchochea shughuli za kiuchumi za mkoa huo.

Tito Mbilinyi, maarufu kama Mwilamu, anasema anashukuru sana kwa kuwa ugeni utakaokuja Ruvuma utasababisha manufaa makubwa ya kiuchumi kwa wananchi wa mkoa huo.

"Hili tamasha sisi wafanyabiashara litatupa manufaa makubwa. Kwenye nyumba za kulala wageni, mama lishe, mwenye teksi atanufaika ugeni ni mkubwa watu zaidi ya 5,000 si mchezo, tunawaomba viongozi wa mkoa wetu wawe wanatutengenezea fursa kama hizi," anasema.

"Rais Samia ni msikivu sana anatujali sisi watu wa sekta binafsi kwa sababu zile changamoto ambazo tunakutana nazo tukimwambia huwa anazitatua haraka sana. Tunamshukuru sana na tunamkaribisha sana Ruvuma.

"Sisi ndio tunajidai kuwa tunalisha mikoa mbalimbali na mataifa mengine yenye uhaba wa chakula. Hili tamasha litatusaidia sana kuinua uchumi wetu. Wananchi wajitokeze kwa wingi kutumia fursa ya tamasha hili," anasema.

Upendo Hosia ambaye ni mdau wa hoteli mkoani humo, anasema taarifa ya ujio wa Rais Samia wamezipokea kwa furaha sana na watahakikisha wanatumia fursa hiyo kuuwezesha mkoa huo kunufaika kiuchumi.

Anasema uchumi wa mkoa



huo umekuwa ukiimarika siku hadi siku kutokana na kupita magari makubwa ya mizigo yanayochukua shehena ya mizigo kusafirisha maeneo mbalimbali.

"Nikiwa kama mama tunampokea kwa mikono miwili. Wanawake wa mkoa huu tumejipanga kumpokea na atafurahi kuona utamaduni wa mkoa wa Ruvuma. wafanyabiashara na wananchi nawaambia kitu kimoja kwamba ujio huu ni muhimu na fursa kwa sababu ugeni huo utaleta maelfu ya watu," anasema.



Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, Mary Makondo, anasema lengo kuu la tamasha hilo ni kuonesha na kuhifadhi urithi wa utamaduni wa makabila mbalimbali ya Tanzania, hasa yale yanayopatikana katika mkoa wa Ruvuma.

Anasema tamasha hilo linatoa jukwaa kwa jamii kushiriki na kuonesha muziki wa kitamaduni, ngoma, sanaa, mavazi ya kitamaduni, vyakula vya asili, mila na desturi za jadi.

Kwa mujibu wa Makondo, tamasha hilo lina umuhimu wa kijamii, kiutamaduni na kiuchumi kwa kuwa litasaidia kuongeza hamasa ya kulinda na kuenzi urithi wa kitamaduni, huku pia likiwavutia watalii wa ndani na nje ya nchi.

Anasema mara nyingi washiriki kutoka mikoa mingine ya Tanzania na hata nje ya nchi, hushiriki tamasha hilo, hivyo kuleta mchanganyiko wa utamaduni wa jamii mbalimbali.

Tamasha la Taifa la Utamaduni ni tukio linaloendelea kuimarika na kushamiri nchini Tanzania, likiwa na lengo kuu la kuadhimisha, kuenzi, na kuhifadhi urithi wa kitamaduni wa taifa.

Anasema tamasha hili hufanyika kila mwaka, likiwakutanisha Watanzania kutoka mikoa mbalimbali na wageni wa kimataifa kwa ajili ya kusherehekea utamaduni wa asili wa nchi. Kwa miaka mingi, tamasha hili limekuwa kiini cha kushirikisha, kujenga na kuimarisha mshikamano wa kitaifa kwa kupitia sanaa na mila za kitamaduni.

**MALENGO YA TAMASHA**

Tamasha la Taifa la Utamaduni lina malengo kadhaa makuu ambayo yamekuwa yakiimarisha umuhimu wake kwa taifa. Kwanza kabisa, lengo kuu ni kukuza na kuenzi urithi wa kitamaduni wa Tanzania. Katika mazingira ya utandawazi na mabadiliko ya kijamii yanayotokea kwa kasi, tamasha hili linachangia kwa kiasi kikubwa katika kuhakikisha kuwa desturi, mila, na sanaa za asili zinadumishwa. Kwa njia hii, vizazi vijavyo vina nafasi ya kujifunza na kujivunia tamaduni zao.

Pili, tamasha hili linatoa jukwaa kwa wasanii wa ndani kuonesha kazi zao, ikiwa ni pamoja na ngoma za asili, michezo ya jukwaani, muziki wa kitamaduni, na sanaa nyingine za kiasili kama vile uchongaji, ususi, na uchoraji.

Hii inatoa nafasi kwa wasanii hawa kupanua soko lao na pia kujifunza mbinu mpya kutoka kwa wenzao, hivyo kukuza tasnia ya sanaa nchini.

Tamasha hilo pia linasaidia kuimarisha umoja wa kitaifa kwa kuwaleta pamoja watu kutoka kabila, dini, na maeneo mbalimbali ya nchi na linaimarisha mshikamano miongoni mwa Watanzania.

Utamaduni ni chombo chenye nguvu kinachoweza kuunganisha jamii, na kupitia tamasha hili, Watanzania wanapata fursa ya kuona na kushiriki katika tamaduni tofauti, hivyo kuongeza uelewa na heshima kwa tofauti zao.

**MAUDHUI NA SHUGHULI**

Tamasha la Taifa la Utamaduni linajumuisha shughuli mbalimbali zinazowakilisha utofauti na utajiri wa urithi wa kitamaduni wa Tanzania.

Muziki wa kitamaduni ni sehemu muhimu ya tamasha hili, ambapo vikundi vya muziki kutoka makabila mbalimbali huonyesha ngoma na nyimbo za jadi, zikiambatana na ala za muziki za asili kama vile ngoma, filimbi, na zeze.

Aidha, maonyesho ya mavazi ya kitamaduni yanachukua nafasi ya kipekee na makabila tofauti huonyesha mavazi yao ya kipekee yanayowakilisha utambulisho wao wa kitamaduni na hiyo husaidia kuhifadhi mitindo ya mavazi ya asili ambayo ina umuhimu mkubwa katika historia ya Tanzania.

Maonyesho ya sanaa za mikono pia ni sehemu muhimu ya tamasha hili kwani wasanii wa kiasili huonyesha kazi zao za mikono kama vile uchongaji wa vinyago, ususi wa vikapu, na uchoraji wa picha za asili. Haya ni maonesho ya ubunifu wa hali ya juu unaowakilisha ustadi wa wasanii wa kiasili wa Tanzania.

Michezo ya jukwaani pia ni sehemu nyingine maarufu ya tamasha na hizi ni pamoja na maigizo ya hadithi za kale za kitamaduni, michezo ya sarakasi, na michezo ya kuigiza inayojikita katika masuala ya kijamii.

Michezo hii hutoa elimu kwa hadhira juu ya maisha, maadili, na mafunzo ya kitamaduni, huku pia ikiburudisha.

**UMUHIMU KWA JAMII**

Tamasha la Taifa la Utamaduni limekuwa na manufaa makubwa kwa jamii ya Kitanzania. Kwanza, linatoa ajira kwa wasanii na wafanyabiashara wa sanaa za mikono.

Wasanii hupata fursa ya kuuza kazi zao kwa hadhira kubwa, ikiwa ni pamoja na watalii na wageni wa kimataifa wanaoshiriki tamasha na hiyo huchangia kukuza uchumi wa ndani na kusaidia wasanii wa asili kuimarisha mapato yao.

Pili, tamasha hili linasaidia katika kuimarisha utalii wa kiutamaduni nchini na watalii kutoka mataifa mbalimbali huvutiwa na utajiri wa kitamaduni wa Tanzania, hivyo tamasha hili linakuwa kivutio kikubwa kwao.

Utalii wa kiutamaduni unachangia kwa kiasi kikubwa katika mapato ya nchi, na tamasha hili limekuwa na mchango mkubwa katika sekta hiyo.

Aidha, tamasha hili linaimarisha utambulisho wa kitaifa na heshima kwa utamaduni kwani watanzania wanaposhiriki na kushuhudia tamaduni zao mbalimbali, wanapata fursa ya kutambua thamani ya urithi wao na hivyo kuwa na fahari ya kuwa sehemu ya jamii ya Kitanzania.

Tamasha hilo pia husaidia kupunguza migogoro ya kikabila kwa kuhamasisha umoja na mshikamano kupitia kusherehekea utofauti wa utamaduni.


# MAISHA

SEPTEMBA 15, 2024

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili

Ukurasa 14


**Maajabu ya asali kwenye ngozi**



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Mbinu za kununua nyumba kwa gharama nafuu



Ukurasa 12

**HARUSI**




# VITO VINAPENDEZA Wakati wa baridi

Ukurasa 13

## WATOTO


### MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| T | ■ | S | H | A | K | A |
| H | ■ | ■ | ■ | K | ■ | S |
| A | ■ | N | Z | I | ■ | H |
| W | A | O | ■ | L | A | O |
| A | ■ | N | O | A | ■ | N |
| B | ■ | D | ■ | ■ | ■ | W |
| U | B | O | S | I | ■ | E |


### FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:


KAA, MBA, BUU, MTI, AWEKE, CHOTA, OBAMA, KUMBE, ASHINDE, PAMBANA

### TOA TOFAUTI 5




### AMSHA AKILI


TAFUTA NJIA KUTOKA A KWENDA B




## PAKA RANGI



### CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO Juma na rafiki yake John walikuwa wakitembea pembeni ya barabara wakielekea shambani. Wakati wakikaribia shambani, Juma alimuona ndege akipaa angani huku akiyumbayumba kwa madaha.Juma alifurahi sana na kuanza kumuuliza rafiki yake.

**Juma:** Ona yule ndege anaruka kwa furaha

**John:** Nimefurahi baba kasema ukimuona ndege ana furaha atakuwa na makinda.

**Juma:** Kwani ndege sawa na mnazi una makinda?

**John:** Hapana ila watoto wa ndege wanaitwa makinda na sio mnazi.

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Dada wa kazi ni mama bora kuliko binti yako!

KARIBU tena msomaji wangu tuelimishane juu ya maisha yalivyo kila uchao. Ndoa nyingi zinakufa mapema kutokana na msingi mbovu wa malezi. Hebu tafahari haya nitakayoeleza hapa upate majibu.

Kuzaa ni tofauti ni malezi na matunzo ni tofauti na kulea. Kulea ni kuongoza, kulea ni kuelekeza, ni kumuandaa mtoto wako. Na aliyepewa jukumu la kulea ni mwanamke. Mwanamume halei bali anatoa matunzo.

Kinamama ni walezi wa mabinti na vijana. Kwenye familia zetu tunaangalia mama si tu jamii inayotuzunguka. Na shetani akitaka kuua familia atamtumia mwanamke.

Atampumbaza ili atoke kwenye nafasi yake ya ulezi. Atasahau ya kwamba hao watoto wanapaswa kuongozwa na yeye, anasahau kwamba yeye ana wajibu wa kulia na kupiga magoti kwa ajili ya watoto wake. Maana hata maandiko ya Mungu yanasema msinililie mimi, jalilieni ninyi na watoto wenu.

Mwenye wajibu wa kulia kwa ajili ya watoto ni mwanamke! Ila adui hupambana kumtoa kwenye nafasi yake kama mlezi kwani anafahamu ana wajibu. Dunia inazungumza kwamba mwanamke akiwa mpumbavu ni mzigo wa mamaye.

> **Msaidie usimpendelee, usimhurumie. Usimwozeshe kwa sababu ya vitu kama vile nyumba, gari. Wazazi acheni kuozesha mabinti kwa ajili ya vitu.**

Si kwamba anadharauliwa mwanamke, bali inakumbusha majukumu. Methali 10:1 "Mwana mwenye hekima humfurahisha babaye; Bali mwana mpumbavu ni mzigo kwa mamaye".

Mfano baba amembeba mtoto akalia pengine amepata haja ndogo, utamsikia anamwambia mama; "unafanya nini bana, hebu njoo mchukue mtoto". Mtoto akiharibikiwa lawama za malezi hutupiwa mama. Eti ni tabia za mama yake. Ila akifanya vizuri, akifanikiwa baba hutamba, huyu ndio mtoto wangu!

Hapo inaonesha jukumu la kulea na kuongoza ni la mwanamke. Mama anapaswa kujifunza jinsi ya kufuatiliwa watoto wake. Kuwa kwenye nafasi ya kuwa rafiki na mwanao.

Mzazi hapaswi kukaa pembeni katika maisha ya mtoto wake. Nafasi ya kwanza ni mzazi kama mzazi lakini nafasi ya pili ni rafiki. Chunguza tabia, usitetee tabia ya uovu ya mtoto wako.

Rafiki hujua siri nyingi za rafiki yake. Lakini mzazi anaweza asijue mwanaye anapitia nini. Lakini rafiki atajua mtoto wa fulani anapitia nini. Ndiyo maana inasisitizwa hapa kwamba kuwa rafiki na mtoto wako.

Utakapokuwa rafiki yake, hataweza kupitia changamoto anazopitia kwa sababu wewe ni rafiki yake atakushirikisha. Kinababa wengi, wamama wengi wameishia kwenye nafasi ya wazazi.

Pamoja na kwamba vitabu vya dini vinatuambia tuwakanye watoto, ikibidi kupiga, kuna wakati wazazi wanapaswa kuwa rafiki nao. Usipokuwa rafiki kwa mtoto wako atapata rafiki wa nje.

Huyo wa nje atamshauri nini? Hawezi kukueleza kwa sababu umebaki na nafasi ya mzazi na kazi moja ni kukemea bila kutambua ya kuwa yapo mambo anapitia usiyoyajua. Lea mtoto wako, simama kama mama, chunguza anayopitia. Alikuwa na nafasi nzuri darasani ameshuka wala hujiulizi kwa nini?

Kuna wakati lazima mama awe rafiki, vinginevyo hana wa kumshauri.Rafiki wa nje anaweza kumharibu. Huu ni wakati wa kizazi hatari na shetani ni mharibifu namba moja!

Binti mlee mwenyewe mama, ukiweka jukumu hilo pembeni usije mlaumu mtu yeyote huko baadaye. Wengi ndio wale wakiolewa wanarudishwa kwa wazazi wao, kisa hawajui kupika, usafi wa nyumba (kudeki, kufua n.k). Wengine hata kutandika kitanda ni mtihani mkubwa.

Ndoa si mapenzi tu bali vipo vikolombwezo vingi vikiwemo nilivyotaja hapo juu. Ndoa ni jukumu, ni wajibu. Mfundishe binti awe rafiki wa mama wa mume yaani mama mkwe.

Msaidie usimpendelee, usimhurumie. Usimwozeshe kwa sababu ya vitu kama vile nyumba, gari. Wazazi acheni kuozesha mabinti kwa ajili ya vitu.

Mabinti wengi wanaingia kwenye ndoa lakini muda mfupi baadaye wanatoka au kuachika kwa sababu msingi wa malezi/makuzi yao ulikuwa na mapungufu mengi. Neno la Mungu linasema, Zaburi 11: 3 "Kama misingi ikiharibika, Mwenye haki atafanya nini?"

Wengi wamebahatika kufunga ndoa nzuri zenye gharama kubwa lakini baada ya mtoto wa kwanza tu, tafrani ndani ya ndoa zinaanza. Kumbe kule kwa wazazi wake binti alikuwa hafanyi chochote. Kazi zote za nyumbani alikuwa akifanya dada wa kazi. Swali, kwa nini dada huyu asiwe mama bora baadaye?

***Je, una maoni, Kisa? Ujumbe mfupi 0715268581. Namba ipo pia WhatsApp.***

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi

# Ukisikia usije mjini ndiyo hii ya Mbowe na Polisi

SEPTEMBA 11, mwaka huu, Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, alitangaza maandamano ya kudai uhai wa wanachama na viongozi mbalimbali wa chama hicho waliopotezwa.

Bila kujali athari zitakazojitokeza, amenukuliwa akisema hadi kufikia Septemba 21, 2024 wanatarajia waone hatua za watu kuwajibika, kuwarejesha waliotekwa na viongozi kadhaa kujiuzulu.

La sivyo! kama hawatochukuliana hatua wenyewe kwa wenyewe, basi wao kuanzia Septemba 23 katika Jiji lote la Dar es Salaam, kila kata kila mtaa, wawe tayari kwa maandamano makubwa.

Wakati Mbowe akiweka msimamo huo, Jeshi la Polisi kupitia kwa msemaji wake, Naibu Kamishna (DCP) David Misime, limesema kwa hatua hiyo waliyofikia, wanajiuliza na wanaendelea kufuatilia na uchunguzi kwa nini CHADEMA inataka kuwatoa kwenye reli ya hatua za kiupelelezi zinazoendelea?

Hatua hiyo ni baada ya Rais na Amiri Jeshi Mkuu, Samia Suluhu Hassan, kuelekeza au kuagiza vyombo vya uchunguzi, vifanye uchunguzi kisha wawasilishe taarifa kwake.

Polisi wanadai Mbowe anawahamasisha wananchi wa mkoa wa Dar es Salaam wa kata na mitaa yote kuingia barabarani lakini pia anaendelea kuhamasisha wananchi wa kanda mbalimbali nchini, kukutana Dar es Salaam ili kuungana na wakazi wa jiji hilo kuingia barabarani kuanzia Septemba 23.

Aidha, DCP Misime anasema: "Ikumbukwe kuwa mara kadhaa, viongozi na wafuasi wa chama hicho wamekuwa wakipanga kuratibu mikakati mbalimbali na kutoa matamshi yenye lengo la kutaka au la kuleta vurugu nchini ili kuharibu amani ya nchi yetu kwa sababu wanazozijua wenyewe.

"Kutokana na taarifa hiyo, Jeshi la Polisi nchini, linatoa onyo kwa viongozi wa chama hicho kuacha kuendelea kuhamasisha wananchi kujihusisha katika uhalifu huo, na yeyote atakayeingia barabarani atakabiliwa vilivyo kwa mujibu wa sheria za nchi.

"Kwa maana hiyo, maandamano hayo yamepigwa marufuku. Jeshi la Polisi linatoa katazo kwa yeyote aliyealikwa, kuelekezwa kufika Dar es Salaam kutoka mkoa wowote ule kwa ajili ya maandamano hayo asithubutu kufanya hivyo, kwani maandamano hayo ni haramu na hayatafanyika."

Akaenda mbali zaidi akisema: "Mtu asipoteze muda na gharama yake. Jeshi la Polisi linaendelea kutoa rai kwa wananchi wapenda amani kutokubali kurubuniwa, kudanganywa au kushawishiwa kwa namna yoyote ile kushiriki katika maandamano hayo na badala yake waendelee kushirikiana na Jeshi la Polisi kutoa taarifa za viashiria vyovyote vya uvunjifu wa amani."

Wakati huo huo, Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Emmanuel Nchimbi, amesema chama hicho kinalaani utekaji na mauaji nchini humo. Dkt Nchimbi amesema mauaji ya hivi karibuni ya kiongozi wa CHADEMA, Mohammed Kibao, ni jambo la kusikitisha na linatia hofu kwa wananchi.

"Taifa linapita kwenye mtihani wa hofu miongoni mwa wananchi, na hatuwezi kulipuuza hilo. Mtu yeyote anayehatarisha usalama wa raia, mtu yeyote ama kikundi kinachotekeleza matendo ya utekaji hawawezi kuwa na nia njema na CCM," alisema Nchimbi.

Akiliita ni genge la watekaji wenye nia mbaya. Nchimbi amedai kuwa matendo ya utekaji yanafanya na watu wenye nia mbaya ya kufarakanisha taifa. "Jambo la utekaji na mauaji linatoa taswira mbaya kwa CCM. Hivyo hatuwezi kuunga mkono."

Nchimbi, amesema tayari matendo hayo yanafanya raia wasiwe na imani na polisi, na ameonya hilo likendelee litaathiri usalama na ustawi wa nchi kwa ujumla.

"Ni muhimu sisi pamoja na wapinzani kushirikiana ili tusiwape genge la watekaji ushindi. Genge linataka kutufarakanisha."

Kiongozi huyo anasema CCM inaunga mkono kauli ya Rais Samia Suluhu Hassan, kutaka uchunguzi ufanyike. "Niseme kuwa CCM imekerwa kweli kweli na jambo hili... Genge hili la watekaji linaweza kuwa popote, ndani ya CCM, polisi au hata CHADEMA. Muhimu ni kuacha uchunguzi wa kina ufanyike, na majibu yake yapatikane ili hatua zichukuliwe."

Kuhusu hoja ya CHADEMA ya kutaka uchunguzi uongozwe na makachero kutoka mashirika ya kijasusi ya kimataifa kama Scotland Yard ya Uingereza, Dk. Nchimbi anasema CCM itaiunga mkono serikali kama itaona umuhimu wa kushirikisha mashirika ya kimataifa.


***• Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***

# HARUSI









NI siku ya kukumbukwa kwa Peter Mwita baada ya kufunga ndoa na mke wake kipenzi hivi karibuni. sherehe ilifanyika jijini Mwanza. **PICHA: MC SARAGATA**

MITINDO

## VITO VINAPENDEZA
# Wakati wa baridi

WAKATI wa hali ya hewa ya baridi, watu huwa wanavaa nguo nzito ili kupata joto, hivyo husababisha hata uvaaji wa mapambo yenye vito kupungua.

Lakini katika kipindi cha baridi hupaswi kujizuia kuvaa vito vyako, bali unatakiwa kupangilia nguo vizuri ili pambo lako lionekane vyema.

KIDANI

Unashauriwa wakati wa baridi vyema kuweka vito vyako katika hali ya mwonekano mzuri pale unapovaa nguo nzito. Mkufu mrefu wenye kidani chenye ujazo mkubwa kinakupa mwonekano wa kupendeza.

**HERENI ZA KUNG'AA**

Ukiwa na jozi ya hereni za kung'aa humfanya mtu kuonekana mrembo hata katika kipindi cha baridi zaidi. Utang'arisha vazi lolote kwa haraka.

**3. LULU NZURI**

Majira ya baridi madini ya lulu huleta mng'aro maridadi. Ni laini, kwa hivyo hazitakupa mikwaruzo hasa katika kipindi cha baridi.

Pia lulu huenda vizuri na rangi za majira ya baridi kama vile nyeusi, bahari, na nyeusi.


**MAPAMBO MAKUBWA**

Vaa vito vikubwa na vinavyokupa ujasiri hasa ukitumia sweta ambalo linakupa joto.Vaa bangili badala ya vikuku maridadi au shanga ndefu ambazo zitayumba kwenye upepo.





UREMBO



# Maajabu ya asali kwenye ngozi

ASALI ina asili ya kuvuta unyevu kutoka kwenye hewa na kuipa ngozi uwezo wa kuhifadhi unyevu na kuleta faida kwa mtu mwenye ngozi kavu.

Chukua asali mbichi kijiko kimoja cha chai kisha paka usoni, kaa nayo kwa dakika 15 hadi 20 kisha safisha uso wako.

Kutibu kuzuia chunusi

Kutokana na uwezo wa asali katika kuua bakteria na kuvuta uchafu katika matundu ya ngozi asali itakusaidia kutatua tatizo la chunusi.

Chukua asali mbichi kijiko kimoja cha chakula changanya na mafuta ya nazi vijiko viwili changanya mchanganyiko uwe mlaini kisha paka usoni huku ukisugua taratibu kwa kufanya kama viduara huku ukiepuka kufikicha machoni. Ukimaliza kusugua uso na mchanganyiko wako osha uso wako.



**KUTIBU NGOZI**

Asali inatibu nywele kavu zilizopauka na kulainisha ngozi kavu ya kichwa na kutibu muwasho kichwani.

Changanya kijiko kikubwa cha asali na maji ya uvuguvugu kisha paka kichwani, acha kwa muda wa saa moja iwe kama conditioner kisha safisha nywele zako.

Unaweza kuchanganya asali kiasi cha kijiko kimoja mpk viwili katika maji vikombe vitano kisha safishia nywele zako taratibu, yapitishe tu hayo maji kwenye nywele zako ambazo ni safi.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Dagaa wa Zanzibar

DAGAA wa nyama au maarufu kama dagaa wa Zanzibar ni mboga inayozidi kujizolea umaarufu kwa utamu wake.

Umaarufu wa dagaa hawa unatokana na uwezo wake wa kuhifadhiwa hadi miezi sita bila kuharibika na ni mboga ambayo inaweza kuliwa na aina yoyote ya chakula.

Mahitaji

Kitunguu maji na saumu, mafuta ya kupikia, nyanya, kitunguu, karoti, pilipili hoho, chumvi, nazi, limao, dagaa na bamia au nyanya chungu chache.

Jinsi ya kupika

Chukua dagaa wako na loweka kwa muda kwenye maji safi ili walainike kwanza kabla ya kuanza kuwapika na baada ya kulowana watoe wachuje maji kidogo kabla ya kuanza kuwaunga.

Bandika sufuria na weka mafuta, anza kukaangisha vitunguu maji na kisha weka kitunguu maji na saumu, vikianza kuwa vya kahawia, weka nyanya, chumvi, kamulia kipande cha limao na funika.





Zikikaribia kuiva weka weka karoti, pilipili hoho, nyanya chungu na bamia na maji kidogo kisha onja chumvi kama imekolea kisha funika.

Baada ya mchanganiko wako kuchemka weka tui la nazi na acha lichemke hadi kupata rojo unayotaka kabla ya kuepua na mboga yako itakuwa tayari kwa kuliwa na wali au ugali.

Mwisho

MAISHA NI NYUMBA

Na Restuta James

## Yajue matumizi mengine ya kontena

WATU wengi wanatumia kasha au kontena, linalotumika kusafirisha bidhaa melini kuhifadhia mizigo ya kibiashara hasa saruji kwa wanaofanya biashara hiyo.

Wengine ambao ni wengi wanaoamua kubadilisha kabisa matumizi ya kontena, huyatengeneza kuwa ofisi na ni wachache ambao huyarekebisha kuwa nyumba au makazi ya kudumu.

Ukurasa huu unakuletea namna ambavyo kontena linaweza kubadilishwa na kuwa makazi ya kudumu au ya muda mijini na vijijini.

Wataalamu wa mapambo ya ndani wanaeleza kuwa kontena likirekebishwa vizuri linafaa kuwa makazi na hasa kwa ajili ya mapumziko (vacation).


Hata hivyo, wanaeleza kuwa ‘finishing’ ndiyo itakayofanya kontena liwe na mwonekano mzuri wa makazi.

Suzan Paul, anasema mwonekano mzuri wa kontena utabebwa na vioo, uezekaji, rangi, varanda itakayowekwa na mpangilio wa bustani hasa nyasi.

“Kingine muhimu ni samani na kiyoyozi kwa mikoa yenye joto. Ukiangalia mtandaoni utaona jinsi ambavyo wenzetu kwenye nchi nyingine wanavyoyabadilisha na kuwa na mwonekano unaovutia,” anasema Suzan.

Anasema jambo la msingi la kuzingatia ni uezekaji mzuri kwani kontena likinyeshewa na mvua kwa muda mrefu linaweza kutoboka na kuanza kuvuja.

“Mbali ya kutumia kama nyumba na ofisi, unaweza kulifanya kontena kuwa eneo la kuogelea yaani ‘swimming pool.’ Kwa wenye maeneo makubwa, unaweza kujenga nyumba kubwa nzuri ya kuishi halafu ukatumia kontena kuengeneza jiko la nje au nyumba ndogo ya vijana au sehemu yako ya mapumziko,” anasema.





# Mbinu za kununua nyumba kwa gharama nafuu

UMILIKI wa nyumba ni kitu muhimu kwa mwanadamu kwa kuwa kinampa uhakika wa malazi. Nyumba ya kumiliki inaweza kuwa ya kujenga mwenyewe au kuinunua kutoka kwa mtu binafsi au kampuni.

Kama mtu anataka kumiliki nyumba na ana fedha, hivyo anataka kununua, moja ya vitu muhimu ni kuwa na mbinu bora za mazungumzo hasa wakati wa kununua.

Mbinu hizo za mazungumzo ndizo zitakusaidia kukamilisha mipango yako kwenye kuwekeza kwa kununua nyumba au kiwanja.

Mtaalam wa uwekezaji kwenye sekta hiyo, Khamis Shaban, anasema mtu anapohitaji kununua nyumba kwa gharama nafuu, kuna njia ambazo anapaswa kuzifuata.

Moja ya njia hizo, anasema ni kuhakikisha unajipanga na kufahamu kanuni za uwekezaji kabla ya kwenda kwenye mazungumzo kwa ajili ya ununuzi wa nyumba husika ikiwamo kuepuka mazungumzo hasi juu ya mtu anayehusika.

“Miongoni mwa maneno ya kukwepa kuyazungumza ni kama kusema ‘basi mtafute atakayeweza kununua kwa bei kubwa, au nani utaweza kumuuzia jengo kama hilo, au basi endelea kutafuta mnunuzi mwingine. Kwa nini unauza bei ya hovyo hivi’. Haya ni baadhi ya maneno yasiyofaa, jitahidi kumuelimisha.

“Wazungumzaji bora hawawezi kutoa kauli za namna hiyo hata kama wanapuuzwa sana kwenye hatua za ununuzi na mauzo bali wataendelea kunyenyekea,” anasema.

Njia nyingine, anasema jitahidi kuchunguza mahitaji au sababu za kuuza nyumba ili ikurahisishie wakati wa majadiliano kwenye ununuzi ambayo yatachangia kuwa na uwezekano mkubwa wa kuipata hata kwa gharama ya chini zaidi.

“Hii ni njia bora zaidi ambayo inasaidia pande zote mbili kunufaika na unatakiwa kuifahamu nyumba husika mnayojadili,” anasisitiza.

Shaban anasema mbinu nyingine ambayo itakusaidia kumteka yule anayekuuzia na akufanyie nafuu ni kuwa makini katika kumsikiliza zaidi kuliko kuzungumza.


“Jifunze kuongea mambo ya msingi tu ya kusaidia kufikia hatua nzuri ya mpango wenu na hakikisha unayoyaongea ni ukweli mtupu, na wakati sahihi wa kuzungumza ni pale unapotaka kuzungumzia hitaji lako,” anasema.

Anasema kwamba katika mazungumzo hayo unapaswa kuyafanya yawe yenye suluhisho ili hata kama itashindikana kwa wakati mmoja iwe ni nafasi ya kufungua fursa na kuweka uaminifu kwa manunuzi mengine ya usoni.

“Kama utajiridhisha kwamba mazungumzo hayo hayaonyeshi dalili ya wewe kununua nyumba kulingana na mipango uliyokuwa umejiwekea, usilazimishe isipokuwa subiri nyingine. Fursa huzaliwa kila siku, usilazimishe uwe na nyumba leo wakati kesho utapata yenye thamani kubwa na inayouzwa kwa bei nafuu mtaa mwingine,” anasisitiza.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
'SIO SIFA!'
UTEKAJI
TUSITISHANE, HUNA MAMLAKA YOYOTE YA KUNIWAJIBISHA HATA NIKIBOLONGA!
ZILE NDOTO UNAZOOTA UMEGEUKA FARASI, UNAMJUA UNAYEMBEBAGA?
SASA NDUGU YANGU UMEZODOA MACHO HUNA UHAKIKA KAMA MI'OMBA-OMBA AU?!
SINA UHAKIKA KAMA HAYO NI MACHO AU MAYAI!
WEWEEE! ONDOA GARI LAKO LA MKOPO UNATULETEA GIZA MBELE!
HIVI BOSI HAJUI KAMA DALADALA INAYOMPA JEURI NI MALI YAKO?
KAMA VIPI MPELEKEE UMTOE KWENYE RELI KUNGUNI HUYO
LIKIWA KWAKE NI MALI YAKE NDO MAANA NATUKANWA!
...KAMA UNANISIMANGA HUKU UNAZUNGUSHA RAUNDI MI SINA TABU!
SUBIRI MFUKO "UKATE" ALAFU UKAE KAMA MFIWA!
HUYO KWA SEKRETARI NI WAIFU KESHAKUJA KUKIWASHA SIJALALA HOMU SIKU MBILI TU!
NONGWA

HABARI KIMATAIFA

# Papa Francis ashauri mwenye uovu mdogo achaguliwe Marekani

**ROMA,** VATICAN

KIONGOZI wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis amewata Wamarekani kumchagua mtu mwenye uovu mdogo kuwa rais katika uchaguzi utakaofanyika Novemba mwaka huu.

Papa Francis amewaita wagombea wote wakuu wa urais wa Marekani kuwa wanapinga maisha na hivyo aliwashauri wapiga kura wa Kikatoliki kuchagua mwenye uovu mdogo wakati watakapokwenda kwenye vituo vya kura.

Papa alisema suala la kutowakaribisha wahamiaji akionekana kumlenga Trump ni dhambi kubwa, na pia alizungumzia msimamo wa Kamala Harris kuhusu uavyaji mimba ni sawa na mauaji.

"Wote wawili wanapinga maisha, awe ni yule anayewafukuza wahamiaji, au awe ndiye anayeua watoto," alisema Papa Francis.

Alitoa ushauri huo usio wa moja kwa moja juzi katika mkutano wa waandishi wa habari alipohitimisha ziara ya siku 12 katika nchi za kusini mashariki mwa Asia.

Hata hivyo, Papa Francis hakumtaja Harris wala Trump kwa jina katika maoni yake.

Wakatoliki wa Marekani ni milioni 52 kati ya bilioni 1.4 duniani kote.

Papa Francis aliombwa kuwashauri wapiga kura wa Kikatoliki wa Marekani wakati wa mkutano wa waandishi wa habari ndani ya ndege na kwenye mazungumzo yake alisema kwamba yeye si Mmarekani.

Lakini aliwahimiza Wamarekani kupiga kura.


"Kutokupiga kura ni jambo baya. Sio vizuri. Ni lazima upige kura," alisema.

"Lazima uchague uovu mdogo zaidi. Ni nani mbaya zaidi? Bibi huyo, au bwana yule? Sijui. Kila mtu, lazima afikiri na kufanya hivyo." alisisitiza

Papa, mara kwa mara amekosoa uavyaji mimba, ambao umekatazwa na mafundisho ya Kikatoliki, kwa maneno makali.

"Kulazimisha mtoto kutoka tumboni mwa mama ni mauaji kwa sababu kuna maisha huko," aliongeza kiongozi huyo

**BBC**



Rais wa Marekani Joe Biden akiwa na Waziri Mkuu wa Uingereza Kier Starmer katika ikulu ya White House mjini Washington juzi. **PICHA: AP**

# Biden, Sir Keir wapata kigugumizi matumizi ya makombora Ukraine

**WASHINGTON,** MAREKANI

WAZIRI Mkuu wa Uingereza, Sir Keir Starmer, ameshindwa kuelezea kama mkutano wake na Rais wa Marekani, Joe Biden, kumepatikana makubaliano ya kuiruhusu Ukraine kutumia makombora ya masafa marefu kuelekea Russia.

Mazungumzo ya viongozi hao wawili yalifanyika mjini Washington.

Alipoulizwa ikiwa alimshawishi Biden kuiruhusu Ukraine kurusha makombora ya masafa marefu ya Storm Shadow kwenda Russia, Sir Keir alisema walikuwa na majadiliano marefu na yenye tija.

Alisema masuala waliyojadili yanahusu nyanja mbalimbali pamoja na Ukraine, Mashariki ya Kati na muungano wa India na Pacific Indo-Pacific.

Hata hivyo, Ikulu ya White House ilisema kuwa viongozi hao walionesha wasiwasi kuhusu utoaji wa silaha hatari unaofanywa na Iran na Korea Kaskazini kwenda Russia.

**Alipoulizwa ikiwa alimshawishi Biden kuiruhusu Ukraine kurusha makombora ya masafa marefu ya Storm Shadow kwenda Russia, Sir Keir alisema walikuwa na majadiliano marefu na yenye tija.**

Awali Rais wa Russia, Vladimir Putin aliyaonya mataifa ya Magharibi kutoiruhusu Ukraine kurusha makombora ya masafa marefu kuelekea Russia, kwani kufanya hivyo ni kuingia vitani moja kwa moja.

Putin alisema hatua kama hiyo itamaanisha ushiriki wa moja kwa moja wa Nato katika vita vya Ukraine.

Akihutubia wanahabari kabla ya mkutano huo, Sir Keir alisema hafikirii sana kuhusu Vladimir Putin.

Kufikia sasa, Marekani na Uingereza hazijaipa Ukraine ruhusa ya kutumia makombora ya masafa marefu katika mapigano yake na Russia, hofu ya kuongezeka kwa vita.

Hata hivyo rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky, kila mara alitoa wito kwa washirika wake wa Magharibi kuidhinisha matumizi hayo akisema ndiyo njia pekee ya kukomesha vita.

Tangu Russia ilipoivamia Ukraine mnamo Februari 2022, miji ya Ukraine na maeneo ya mstari wa mbele yamekuwa yakishambuliwa kila siku.

**BBC**

# Afrika Kusini kuendelea kuibana Israel

**FRETOWN,** AFRIKA KUSINI

ARIKA KUSINI imesema inaendelea na kesi yake iliyofunguliwa katika Mahakama ya Kimataifa ya Haki (ICJ), dhidi ya Israel ikiishutumu kufanya mauaji ya halaiki katika Ukanda wa Gaza.

Rais, Cyril Ramaphosa, amesema nchi yake itawasilisha malalamiko Oktoba, mwaka huu.

Afrika Kusini ilifungua kesi hiyo Desemba 2023, ikieleza kwamba vita vilivyoanzishwa na Israel katika Ukanda wa Gaza ni sawa na mauaji ya halaiki na vinakiuka Mkataba wa Umoja wa Mataifa juu ya mauaji ya kimbari ya mwaka 1948.

Israel ilipinga mashtaka hayo ikidai ni jaribio la dharau la kunyima haki yake ya kimsingi ya kujilinda.

"Sisi tunajali maoni ya wengine," alisema Rais Ramaphosa, alipoulizwa kuhusu kesi hiyo wakati wa mkutano na waandishi wa habari.

"Tumedhamiria kusogeza faili yetu mbele." Alisisitiza.

Amebaini kwamba kesi hiyo itawasilishwa mwezi Oktoba mjini Hague nchini Uholanzi.

Aliongeza kuwa wanaendelea kusihi kwamba mauaji ya kimbari lazima yakome na kwamba lazima kuwe na usitishaji vita na Hamas lazima warejeshwe mateka.

Nchi kadhaa ikiwemo Uturuki zimejiunga katika kesi hiyo kuisaidia Afrika Kusini.

Hukumu itakayotolewa na ICJ ipo kisheria lakini haina uwezo wa kulazimisha kutekelezwa na nchi husika.

Uamuzi wa iwapo Israel inatekeleza mauaji ya halaiki au la unaweza kuchukua miaka mingi na Afrika Kusini mara kadhaa imeitaka ICJ kuagiza hatua za muda zichukuliwe dhidi ya Israel, katika kukabiliana na hali mbaya ya kibinadamu katika Ukanda wa Gaza.

Mnamo mwezi wa Januari, ICJ iliitaka Israeli kuzuia kitendo chochote kinachowezekana cha mauaji ya halaiki na kuruhusu ufikiaji wa misaada ya kibinadamu katika Ukanda wa Gaza.

Oktoba 7, mwaka jana wapiganaji wa Hamas waliingia kwenye ardhi ya Israel kutoka Gaza walifanya shambulio ambalo lilisababisha vifo vya watu 1,205 wengi wao wakiwa raia.

Katika kulipiza kisasi, Israel imeua watu 41,118 mpaka kufikia sasa, kulingana na ripoti kutoka Wizara ya Afya ya serikali ya Hamas.

**RFI**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Pesa zimeisha kimada kamkimbia jamaa



**Na Adam Fungamwango**

IMEKUWA ikisisitizwa tangu enzi na enzi kuwa mapenzi si pesa wala mali, bali ni dhamana ya moyo wa mtu. Ni kweli kabisa mapenzi yanatoka moyoni, na siku zote mapenzi ya pesa au mali si mapenzi ya kweli.

Hapa tuelewane. Ni hivi, mapenzi yanaanza kwanza, halafu vitu vingine vyote vinafuatia. Si pesa au mali ndiyo zinaanza kutengeneza msingi wa mapenzi. Hapo mapenzi hakuna kabisa. Lakini pamoja na hayo yote, hata penzi la kweli nalo linarutubishwa na pesa na mali.

Mwanamke anapompenda mwanaMume, baadhi ya vitu ambavyo anaamini atavipata ni upendo wa kweli, kujaliwa, kutuzwa na kupewa mahitaji yake kwa msingi.

Kwa maana hiyo siyo kwamba mapenzi siyo pesa wala mali, basi mwanaume akae tu asitafute kazi kwa sababu huo si msingi wa mapenzi, utakimbiwa tu.

Mwanamke hata kama atakupenda vipi, mwanaMume ukishaanza kuwa huwezi tena kumhudUmia vile ambavyo anahitaji, ataondoka. Hakuzaliwa na wewe. Hili ni somo gumu na la kusikitisha ambalo wanaume wote lazima walielewe.

Mwanamke anakupenda, sawa, lakini kula ya shida, kulala kwa tabu, nguo kwake matatizo, saluni kama kituo cha polisi, hata mafuta, poda, losheni, wala vipodozi, atavumilia lakini itafika mwisho ataondoka.

Ataondoka si kwamba hakupendi bali ni kwa sababu yeye anataka kupata mahitaji yake. Mara nyingi wanawake ana aibu kuliko wanaume. Mtu aliyekuwa anavaa vizuri, kula vizuri, amenawiri, ngozi laini kwa vipodozi, leo ageuke na kupauka! Anakuwa simulizi mitaani. Hilo ndilo linalowafanya kukata tamaa na kuamua kuondoka.

Kusemwa, kutetwa, kuchekwa na wenzake si kitu ambacho wanawake wanapendezewa nacho. Atakuacha kwa sababu anaona aibu, si kwa sababu hakupendi. Hapa ndipo unapokuja ule msemo wa watoto wa mjini siku hizo kuwa, 'mwaume tafuta pesa, mengine yote yatafuata baadaye.' Kama una mali kama shamba, nyumba, mifugo nayo ni vizuri zaidi, huwezi kutetereka.

Ukiacha wa aina hiyo, wanakuja wanawake ambao wako kimaslahi zaidi. Hawa hawana mapenzi yoyote. Wako kwenye staili ya nipe kikupe. Yuko na mwanamume kwa sababu anapata mradi wake. Huyu anaweza kuondoka muda wowote akipata mtu mwenye pesa au mali zaidi ya aliye naye.

Anaweza kukuacha hata kama una kazi, kwa sababu amekutana na mtu mwenye kipato kikubwa zaidi. Usiombe sasa ndiyo ukawa na mwanamke wa aina hii halafu ukatimuliwa kazi yupo mikononi mwako. Ataondoka kwa dharau, mbwembwe na vituko kama huyu hapa aliyeimbwa na bendi ya Simba Wanyika.

Bendi hii iliyokuwa na wanamuziki wa Kitanzania waliokuwa wakifanya kazi zao nchini Kenya, katikati ya miaka ya 1970, moja kati ya nyimbo nyingi walizotunga ni 'Kimada.'

"Kimada wangu ooo kimada, umeanza madharau, kwa kuwa kazi sina, pesa sina kijana, nakumbuka, tuliishi nawe, ulinikuna nina madaraka kijana, kijana mama, penzi letu lilikuwa la furaha, hata sikudhania tutatengana mimi na wewe."

**Ataondoka si kwamba hakupendi bali ni kwa sababu yeye anataka kupata mahitaji yake. Mara nyingi wanawake ana aibu kuliko wanaume. Mtu aliyekuwa anavaa vizuri, kula vizuri, amenawiri, ngozi laini kwa vipodozi, leo ageuke na kupauka! Anakuwa simulizi mitaani. Hilo ndilo linalowafanya kukata tamaa na kuamua kuondoka.**

Jamaa alikuwa na mpenzi wake ambaye waliishi kwa furaha sana, lakini hakudhania kuwa yupo kimaslahi. Mwanaume alikuwa na cheo, lakini kazi amefukuzwa na mwanamke badala ya kumfariji, akaamua kukimbia.

"Iyelelee oooo iyoo mama aaa. Iyelelee oooh mama aaa. Iyelelee oooh mama aaa.

Madaraka sina, kimada wangu kanikimbia mama, anaranda na rafiki zangu mitaani.

Anaranda na rafiki zangu oooh mitaani mama. Madaraka sina, kimada wangu kanikimbia mama, anaranda na rafiki zangu mitaani

Anaranda na rafiki zangu oooh mitaani eeee."

Hapa tunaona kuwa yule mpenzi wake kwa sasa anaranda na rafiki zake au wapambe wake wakati huo. Sasa ndiyo mwanamke wao. Hapa pia kuna kitu cha kujifunza. Kumbe ukiwa huna pesa hata marafiki wanakugeuka, siyo mpenzi tu.

"Nisaidiwe na na nani, rafiki zangu siwaoni eee, inabaki ni vicheko nipitapo eee.

Inabaki ooh ni vicheko nipitapo eee. Inabaki ni vicheko nipitapo eee."

Jamaa sasa analia ukiwa, hana mpenzi wala rafiki, badala yake wote waliokuwa wakimheshimu sasa wanamcheka kila anapopita."

Haya ndiyo maisha ya hapa duniani, kuwa makini, akili kichwani mwako, ukichelewa umeachwa feri.

**Tume meseji 0716 350534**

# Kijaji asifu kiwanda cha mbolea inayochakatwa kutokana na taka

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Ashatu Kijaji, ametembelea na kukagua mradi wa kuchakata taka kwa ajili ya mbolea ya asili ulioko Mabwepande, Kinondoni mkoani Dar es Salaam.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo juzi, Dk. Kijaji alisema mradi huo utasaidia kutunza mazingira kwa kuwa jamii itapata nafasi ya kukusanya taka na kuzielekeza katika kiwanda hicho na kuepusha kuzagaa ovyo.

Kutokana na uwapo wa kiwanda hicho, Dk. Kijaji aliitaka Manispaa ya Kinondoni inayoendesha mradi huo, kushirikiana na wadau wa sekta binafsi katika uendeshaji.

Waziri Dk. Kijaji aliwataka kuwatengenezea miundombinu wananchi kutenganisha taka wanapozipeleka kwenye mradi huo kwa ajili ya kuchakatwa na kuwa mbolea.

Alisema kushirikiana na wadau hao kutasaidia kuongeza ufanisi wa kazi ya kukusanya taka na kwamba eneo hilo la kiwanda ni kubwa na bado halijapata kutumika inavyotakiwa.

Dk. Kijaji aliielekeza manispaa hiyo kuboresha mazingira ya eneo hilo la ukusanyaji wa taka kwa ajili ya kuchakatwa na kuwa mbolea ya asili ili kuwa rafiki kwa wafanyakazi.

Sambamba na hilo, alisema wafanyakazi wa kiwanda hicho kupatiwa vifaa vya kujikinga na hewa inayotokana na taka zinazikusanywa ili kulinda afya zao.

Naibu Katibu Mkuu (Mazingira), Christina Mndeme, alitoa wito wa kupanua wigo wa mradi huo iwe kukusanya taka nyingi zaidi na kuzalisha bidhaa zingine zaidi ya mbolea.

Alisema zinahitajika taka nyingi ziwe mali badala ya kuishia zaidi kwenye madampo kwa kuwa uzalishaji wa taka jijini ni mkubwa kuliko zinazopelekwa kwenye mradi huo.

Mradi wa mbolea ya asili unatekelezwa kwa ufadhili wa Jiji la Hamburg la Ujerumani lililoingia makubaliano na serikali ya Tanzania kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni nne.

Katika ziara hiyo, mbali na Mndeme, Waziri Kijaji aliambatana na Mkurugenzi wa Kituo cha Kitaifa cha Ufuatailiaji wa Kaboni (NCMC), Prof. Eliakim Zahabu na Ofisa Mazingira Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Dk. Kanizio Manyika.



# Wakumbushwa kuishi kiapo cha taaluma

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MGANGA Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Thomas Lutachunzibwa, amewataka wataalamu wa afya kufanya kazi kwa bidii kwa kuzingatia kiapo cha taaluma bila kuweka mbele maslahi.

Dk. Lutachunzibwa aliyasema hayo jana wakati akifunga mafunzo ya siku mbili ya kudhibiti matukio ya sumu kwa wataalamu wa afya Mkoa wa Dodoma, yaliyoandaliwa na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA).

"Kwenye taaluma ya afya tuna viapo ambavyo vinatanguliza mbele utu na kuwasaidia watu na si kutanguliza fedha mbele, hivyo tuchape kazi kila mtu ana jukumu la kutumia elimu hii tuliyoipata kuisaidia jamii yetu ya watanzania kuzuia na kupambana na matukio ya sumu," alisema.

Dk. Lutachunzibwa aliishukuru GCLA kupitia Kituo cha Taifa cha Kudhibiti Matukio ya Sumu kwa kuwezesha mafunzo hayo kwa sababu, yanawajengea wataalam wa afya uwezo wa kupambana na matukio ya sumu yanapotokea.

Mkuu wa Kituo cha Taifa cha Kudhibiti Matukio ya Sumu kutoka GCLA, Yohana Goshashy, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo madaktari, wataalamu wa maabara na wauguzi kuweza kukabiliana na matukio ya dharura ya sumu.

"Katika Mkoa wa Dodoma kumekuwa na ongezeko la matukio ya sumu, hapo awali Dodoma haikuwa katika mikoa 10 yenye matukio ya sumu, lakini kwa sasa imeingia kwenye orodha hiyo. Jambo hili limetusukuma kutoa elimu hii ili kusaidia kuzuia na kudhibiti matukio hayo" alisema Goshashy.

Washiriki wa mafunzo hayo Dk. Teodora Mwasu na Dk. Misana Yango, walipongeza GCLA kwa kuwapa elimu ambayo itawaongezea ufanisi maradufu katika kupambana na kudhibiti matukio ya sumu kwa mkoa huo.

# HADITHI

BAADA ya kumaliza masomo yake ya kidato nne na kushindwa kuendelea na masomo kutokana hali duni ya wazazi wake, Shani alitakiwa kuolewa. Akakubali, lakini ni kwa yule ambaye anampenda.
Haikuwa hivyo, kwani baba yake mzee Chilambo alimlazimisha aolewe na mwanamume mwenye uwezo, mali na fedha ili asiende kuteseka.
Tatizo likaanzia hapo, mwenye pesa hakupendwa na Shani, asiye na uwezo alikuwa kwenye moyo wake. Baba anamtaka mwenye uwezo. Jambo hili linazua mgogoro mkubwa kwenye familia tatu, za binti na wachumba wawili. Nini kitatokea. Usikose kila nakala ya gazeti hili.

# Aka Simtaki-11

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

"Hivi huna habari?" Mbea huyo alimnong'oneza sikioni ili wengine wasisikie. "Habari gani tena?"


"Za Shukuru?!!" Kusikia jina hilo, Shani alishtuka. Hakusema kitu akabaki anamtazama shoga yake. "Kumbe yupo hai, hajafa, nimepata taarifa na hivi sasa anapatiwa matibabu ya majeraha tu ya kuanguka, ni mzima dada."

"Ni mzima?" Shani akauliza mwenyewe. Akajiuliza jinsi Shukuru atakapojisikia kama akirejea na kukuta tayari ameshafunga ndoa ya Fotu. Yeye mwenyewe hakuna tayari na ndoa ile ni kwa sababu tu ya baba yake.

Akajiona msaliti. Mtu ambaye aliamua ajitoe uhai kwa ajili yake. Kwa sababu ya kumpenda. Ni upendo gani aliokuwa nayo kwake Shukuru. Binafsi alimpenda sana Shukuru, na anajua Shukuru anampenda sana, ila mazingira ndiyo yamekataa.

Wakati huo huo, alikuja mama mmoja akamwinua kwa ajili ya kumpeleka akashikane mikono na mpenzi wake kabla ndoa haijafungwa. Mawazo yalikuwa mengi kichwani. Hakujua afanye nini. Akanyanyuka kwa tabu. Akatembea kwa kujikongoja. Akapelekwa kwenye chumba ambayo aliwepo Fotu. Ndiyo mara ya kwanza alikuwa anamuona. Alikuwa kijana wa kitajiri aliyependeza kwa suti kali na viatu nyeusi vilivyong'aa kwa dawa.

Hiyo haikumshawishi Shani. Kijana alisimama kwenda kumlaki mke mtarajiwa. Kabla hata hajafanya hivyo, Shani alianguka chini pepe yake bila kuguswa na mtu. Kila mmoja alitahayari. Watu wazima walimkimbilia kwenda kujaribu kumpa huduma ya kwanza. Mzee mmoja alipeleka sikio lake kwenye moyo. Aliposikiliza kwa sekunde kadhaa, akamwita mzee Chilambo. Akamnong'oneza kitu. Mzee Chilambo ghafla alitoka hapo na kuhangaika kuitafuta simu yake. Akapiga kwa lengo na kuita bodaboda ambayo nyuma yake ilifungwa kama mkokoteni, na mjini zinafahamika kama Toyo. Kijiji hapo ndiyo iliyotumika kupeleka wagonjwa wasiojiweza kukaa kwenye basikeli au bodaboda ya kawaida kupelewa zahanati ya kijiji. Toyo hiyo ya mwanakijiji mmoja ilitumika kupeleka wasiojiweza, au kusafirisha maiti. Alifanya hivyo kwa malipo. Lakini kutokana na kuwa na yeye ni mwanakijiji, aliweza kuifanya kazi hiyo hata kama mwenye kuhitaji hana pesa kwa wakati huo, na angelipa baadaye. Iliwasili baada ya dakika 20 na moja kwa moja alipelekwa kwenye zahanati.




**"Mzee wangu, muokoe binti yako. Amesema anataka jibu kukoka kwako. Kama ukimlazimisha kuolewa na yule kijana basi anachomoa dripu ya damu aliyotundikwa ili afe." Sauti mzee Kilimba ilipenya vyema masikioni mwa mzee Chilambo.**

Fotu naye alianguka chini kwa mshtuko kwa kile kilichotokea pamoja na aibu pia. Alishaambiwa tangu mapema kuwa msichana hakuwa radhi kuolewa na yeye. Penye wengi kuna mengi. Yeye mwenyewe, wazazi wa ndugu zake walidokezewa kisa cha bi harusi kuanguka. Amelazimishwa kuolewa. Hakumtaka Fotu, na amembiwa kuwa mpenzi wake Shukuru ambaye kila mmoja alijua alitoka pale alipojinyonga akiwa maiti ila ilifichwa tu, amezinduka kwenye hospitali ya mkoa na hajafa kama ilivyosemekana au kuaminika. Waliambiwa kijana huyo alijinyonga kwa kumkosa Shani ambaye aliambiwa anaolewa na kijana wao. Binti naye hali yake haijulikani kwa sababu mwanaume huyo. Kwa bahati nzuri Fotu alizinduka akiwa hapo hapo baada ya juhudi kubwa za ndugu jamaa na marafiki, lakini kwa Shani hali ilikuwa mbaya.

Fotu aliondoka na ndugu zake, huku ndugu na wazazi wa bi harusi walikimbizana zahanati. Naye pia iliamriwa apelekwe hospitali ya mkoa wa Mpanda.

******************************

"Mzee wangu, muokoe binti yako. Amesema anataka jibu kukoka kwako. Kama ukimlazimisha kuolewa na yule kijana basi anachomoa dripu ya damu aliyotundikwa ili afe." Sauti mzee Kilimba ilipenya vyema masikioni mwa mzee Chilambo.

Alikuwa ameitwa nje ya hospitali ya mkoa wa Mpanda ili kuambiwa ujumbe ambao mzee huyo alitumwa na binti yake Shani.

Wakati akionekana na mshtuko huku kichwa chake kikionekana na mawazo mengi, mzee Kilimba akaendelea.

"Kasema anataka jibu ndani ya masaa matatu, kabla dripu haijaisha. Kama hukujibu lolote basi anejua umekataa na atafanya kama alivyodhamiria."

Ilikuwa ni siku ya tatu baada ya Shani kufikishwa hospitalini na kupatiwa matibabu. Ilionekana yupo hai na alizirai.

Mzee Chilambo hakuongea kitu, akabaki anamtazama mwenzake usoni kama kwamba kuna kiti kizito anajitaji kuongea.

Wakati huo baadhi ya ndugu walikuwa pembeni mwa kitanda cha Shani. Na wakati anamwagiza mzee Kilimba alimwita na kunong'oneza bila wao kujua. Ndipo alipomfuata na kumtoa nje ili asisikie mti yoyote.

"Twende. Nifuate." Akajibu kwa mara ya kwanza. Jibu hilo lilimtisha. Kutokana na utata wa mzee Chilambo, alijua kabisa kuwa anakwenda kulianzisha ndani ya hospitali. Alimfuata wakarudi tena wodini.

Walipofika walikutana na watu watatu walioongeka wodini. Ni Shukuru, baba na mama yake. Walikwenda kumtazama mgonjwa. Ilikuwa ni baada ya Shukuru kuruhusiwa na madaktari. Baada ya kuthibitisha amepona, alipwa ruhusa. Hata hivyo aliambiwa kuwa mpenzi wake naye amelazwa hapo. Aliwaambia ndugu zake warudi nyumbani lakini yeye ni lazima akamuone Shani.

Wazazi wake hawakumkatalia kwa sababu alijua yeye ndiye chanzo cha yote, lakini hawakutaka kumuacha kwenda peke yake.

Wasiwasi wao ulikuwa kwa mzee Chilambo ambaye walijua anaweza kuleta tatizo, lakini kwa sababu Shani alikuwa mgonjwa, na yeye Shukuru ametoka kwenye ugonjwa, walijua anaweza kupoa kidogo.

Mze Chilambo na mwenzake Kilimba walirejea kwenye kitanda alicholazwa Shani. Wote waliokuwepo walishtuka kwani kitendo cha kuwepo Shukuru pale walikuwa kutakuwa na tatizo. Mzee Chilambo alimuona Shukuru na wazazi wake. Hakuonekana kama anataka kuongea lolote, au kuchukia. Alikwenda moja kwa moja kwenye kitanda cha binti yake, akamuinamia na kumong'oneza kitu ambacho hakikusikika kwa yoyote. Shani alionekana kutikisa kichwa kukubali. Aliipomaliza, alisogea nyuma na kumfuata Shukuru ambaye alikuwa amedhohofika kutokana na ugonjwa. Aliogopa lakini hakuweza kusogeza hata mguu wake. Akamshika mkono, anamsogeza taratibu kwenye kitanda cha Shani. Akauchukua mkono wa Shani na kuwashikisha. halafu yeye akaondoa mkono wake. Kilichobakia ni kwamba Shukuru na Shani walibaki wameshikana mikono. Kitu hicho kisababisha ndugu wote wapigwe butwaa. Haikuwa hawaida na wasingeweza kufikiria kuwa ingekuwa rahisi kiasi hicho.

"Mnisikilize kidogo." Aliwaambia. "Nimegundua kuwa sikuwa sahihi. Nilikuwa nadhulumu nafsi za upendo za vijana hawa. Wote ni mashukuda kwa kilichotokea mpaka wote kulazwa hapa. Sitaki mtu yoyote arudi nyuma, au kukumbuka yaliyopita. Mimi hapa leo natamka rasmi kuwa nimekubali Shukuru amuoe binti yangu Shani. Kila kitu, mipango, harusi vitafanyika baada ya hapa. Binti yangu ataruhusiwa baada ya siku mbili. Kijana amesharuhusiwa. Sina la kiongeza, naomba msamaha kwa wote waliokwazika." Akasema kwa sauti ndogo nzito na yenye mamlaka. Akaenda kuwakumbatia wazazi wa Shukuru.

Mikono ya Shukuru na Shani bado ilikuwa imeshikana kwa upendo na husia kali. Kila mmoja alibubujikwa machozi ya furaha wasiamini kile walichikisikia kuwa baada ya kutoka pale hospitali watakwenda kufunga ndoa.

"Shani, pole sana mpenzi." Shukuru alitamka kwa sauti ya upole ya huruma. "Ahsante Shukuru, pole na wewe pia."

**MWISHO**

## HABARI BURUDANI



# YOUNG LUNYA KAANZA SAFARI

RAPA Young Lunya, amesema ameanza safari ya kimataifa baada ya kushirikishwa katika ngoma ya 'Normal Day' ya msanii kutoka Nigeria, DJ Neptune.

Wimbo huo upo katika Albamu mpya ya ke mpya iitwayo Great Ness III, ambayo ameonekana kufanya vizuri kwa mashabiki wa nyimbo za lugha ya Kiswahili.

Ndani ya albamu hiyo kuna ngoma 14 ikiwajumuisha wasanii wengine wa kimataifa Qing Madi, Joeboy na Joshua Baraka kutoka Uganda.



# ALI KIBA HANA KINYONGO

KIONGOZI wa lebo ya King Records, Ali Kiba, amesema anamuunga mkono mdogo wake Abdul Kiba kufanya kolabo na Mbosso ambaye anatoka WCB.

Akizungumza hivi karibuni, Kiba amesema wasanii hao ambao wanatoka lebo tofauti wameishi kama marafiki kwa muda mrefu, hivyo kuamua kufanya kazi pamoja sio jambo la kumshtua.

"Abdul na Mbosso ni marafiki kwa muda mrefu na hata aliponiambia wanafanya kolabo sikumkatalia kwa sababu wao wenyewe wanaona ni jambo zuri, na mimi namuunga mkono," amesema Kiba.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ANTHONY ASITA KUONDOKA UNITED

WINGA wa Brazil, Antony mwenye umri wa miaka 24, anasita kuondoka Manchester United licha ya Fenerbahce kumtaka. ***(ESPN)***

### DILI LA TRIPPIER UTURUKI NDO BASI

KLABU za Super Lig za Uturuki, Istanbul Basaksehir, Fenerbahce, Besiktas na Eyupspor vimekata tamaa kujaribu kumsajili Kieran Trippier baada ya Newcastle United kuweka wazi kuwa wanataka kusalia na beki huyo wa zamani wa Uingereza mwenye umri wa miaka 33. ***(Sky Sports).***

### ASTON VILLA WAMGANDA DURAN

KLABU ya Aston Villa imeonyesha kuwa bado inamuhitaji nyota wake Jhon Duran baada ya hivi karibuni klabu hiyo kukataa ofa ya pauni milioni 40 kwa ajili ya mshambuliaji huyo wa Colombia mwenye umri wa miaka 20 ambaye alikuwa akitakiwa na klabu mbalimbali katika msimu huu wa majira ya joto. (Mirror)

### VIGOGO NEWCASTLE MAMBO SAFI

KOCHA wa Newcastle United, Eddie Howe na Mkurugenzi wa Michezo, Paul Mitchell wametatua tofauti zao na sasa wanaangazia uhamisho wa Januari, ikiwa ni pamoja na kumleta beki wa Crystal Palace, Muingereza Marc Guehi mwenye umri wa miaka 24. ***(Telegraph)***

### MAN UNITED YAMGANDA SANCHEZ

KLABU ya Manchester United inamfuatilia beki wa kulia wa Sevilla, Juanlu Sanchez mwenye umri wa miaka 21. ***(AS)***

### CHELSEA KUJENGA UWANJA MPYA

CHELSEA imefanya mazungumzo kuhusu kuondoka Stamford Bridge na kujenga uwanja mpya katika eneo la Earl's Court. ***(Guardian)***

### SPURS ILIMKATAA CRISTIAN ROMERO

KLABU ya Tottenham Hotspur ilikataa ofa za kumnunua beki wa Argentina, Cristian Romero mwenye umri wa miaka 26, wakati wa dirisha la uhamisho la majira ya joto. ***(TyC Sports)***

### COOPER KUTUA CSKA SOFIA BURE

MLINZI wa Scotland, Liam Cooper mwenye umri wa miaka 33 anakaribia kujiunga na CSKA Sofia kwa uhamisho wa bila malipo baada ya kuondoka Leeds United mwishoni mwa msimu uliopita. ***(Football Insider)***

### EVERTON MBIONI KUNUNULIWA

MFANYABIASHARA wa Marekani, John Textor ana imani kuwa dili la kuinunua Everton linaweza kukamilika baada ya wiki nne. ***(Guardian)***

### MONGAN ATOSWA REA MADRID

ANDY Mongan wa Stockport County amezuiwa kujiunga na timu ya makocha ya Real Madrid baada ya kunyimwa kibali cha kufanya kazi kwa sababu ya kanuni za Brexit. ***(Times)***

### CHUKWUEMEKA KWA MIKOPO

KLABU ya Galatasaray ina nia ya kumsajili winga wa Chelsea mwenye umri wa miaka 20 kutoka England, Carney Chukwuemeka kwa mkopo.***(Teamtalk)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# WAKALA AFICHUA NICO WILLIAMS HAKUTAKA KUIHAMA KLABU YAKE

Nyota huyo alikuwa lulu sokoni akiwindwa na klabu kubwa Ulaya, lakini...

**BARCELONA, Hispania**

WAKALA wa winga wa Athletic Club, Nico Williams amefichua kuwa nyota huyo hakutaka kuihama klabu yake msimu huu wa majira ya joto.

Akiwa na kipengele cha kuuzwa kwa pauni milioni 49 katika mkataba wake, Williams alionekana kama anaweza kuwa miongoni mwa dili kubwa zaidi msimu huu wa kiangazi kwani Arsenal, Chelsea na Barcelona zote zilifukuzia saini yake, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 alikataa ofa zote na kupendelea kubaki Athletic.

Akizungumza na Cadena SER, [redacted]

lakini alimsifu winga huyo kwa kujiamini.

"Kijana huyu amekuwa na mwaka wa ajabu na wa kuvutia, kwangu amethibitisha hilo kwa kuwa, binafsi huyo ni mchezaji bora wa Euro 2024," alisema wakala Felix Tainta.

"Tumekuwa na harakati nyingi, safari nyingi, tuna furaha, lakini kila kitu kimebanwa kwa muda mfupi sana na tunafika mwisho wa soko tukiwa na mkazo.

"Kijana ameamua kubaki mwaka mwingine tupo kwa ajili ya kufanya kazi, kumuunga mkono katika maamuzi yake yote na kumshauri, alitaka kubaki ni ushahidi kuwa mchezaji anapotaka kubaki klabu [redacted]

anaweka bunduki kichwani na kusema 'ondoka nataka uje ninapotaka'.

"Mchezaji na familia wana uhuru kabisa, ni rahisi sana kumshambulia wakala, sisi ndio tunaambulia vipigo vyote. Sisi ni saratani za mpira, lakini wakurugenzi wa michezo wapo wengi ambao hawana klabu na wanakuwa mawakala kwa muda mrefu," alisema Tainta.

Mchezaji mwenzake wa Hispania, Lamine Yamal, rafiki wa karibu wa Williams, amekiri waziwazi nia yake ya kutaka kuungana na winga huyo katika ngazi ya klabu na hivi karibuni alithibitisha nia yake ya kumuona nyota huyo wa Athletic akijiunga naye Barcelona.

# ARTETA: STERLING ANA JAMBO LAKE

**LONDON, England**

MIKEL Arteta amesema mara baada ya kufanya mazungumzo na Raheem Sterling wamekubaliana na nyota wake huyompya kuwa ana jambo la kuthibitisha anapotaka kufufua soka lake.

Arsenal itasafiri hadi Tottenham kwa ajili ya mchezo wa dabi ya London Kaskazini leo Jumapili huku kukiwa na sintofahamu juu ya kikosi chao cha kuanza baada ya nahodha Martin Ødegaard na Riccardo Calafiori wote kupata majeraha wakati wa mechi za kimataifa.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba huenda wawili hao wakakosa mchezo wa Jumapili lakini Arteta alikataa kuwaondoa wachezaji wote wawili kwani Odegaard anafanyiwa uchunguzi zaidi wa tatizo la kifundo cha mguu na Calafiori anauguza jeraha la mguu.

Wakati Declan Rice pia amesimamishwa, mchezaji mmoja ambaye upatikanaji wake haujatiliwa shaka ni Sterling, ambaye alijiunga na Arsenal siku ya mwisho ya usajili kwa mkopo wa msimu kutoka Chelsea katika hatua ambayo iliibuka tu katika saa chache za mwisho za dirisha.

Sterling aliondolewa kwenye kikosi cha kocha wa muda wa England, Lee Carsley na hivyo amekuwa na takriban wiki mbili kuzoea mazingira yake mapya katika kambi ya mazoezi ya Arsenal, Colney.

"Anaonekana mzuri. Ana nguvu nyingi, tabasamu usoni mwake na yuko katika hilo. Anataka kuthibitisha jambo fulani na mtu anapokuwa na hilo tumboni mwake unalihisi mara moja," alisema Arteta katika mkutano na wanahabari kuhusu. Ijumaa.

"Ni wazi sihitaji kujua kitu kingine chochote kuhusu ubora wake na nini anaweza kuleta kwenye timu.

"Katika maisha yake binafsi mambo mengi yamebadilika lakini kwa mchezaji huyo nilimshangaa sana, simu ya kwanza niliyopigiwa naye nilijua ndani ya sekunde kumi za kwanza lazima tumlete kwa sababu alikuwa akitaka sana.

"Hiyo ndiyo ilikuwa swali langu pekee: 'yuko katika hatua gani katika kazi yake?', Lakini baada ya sekunde 10, nilijua tayari kabla ya maswali yaliyofuata kwamba tulimhitaji hapa.

"Ninachokiona ni njaa. Ni mchezaji anayetaka kucheza kila dakika ya kila mchezo. Wakati si hivyo, hana furaha. Anataka kucheza kila siku na naona hivyo.

"Kujitolea kwake na kiwango cha nguvu anacholeta kwenye timu ni nyongeza kubwa. Unaweza kuhisi inapita mlangoni. Tuko vizuri zaidi naye. Atatufanya tuwe bora zaidi."

Arteta alitia saini mkataba mpya wa miaka mitatu na nusu siku ya Alhamisi ambao unamunganisha na klabu hiyo hadi 2027.

Alipoulizwa kama kungekuwa na kazi nyingine ambayo angeiacha, Arteta alisema: "Hapana, uhusiano wa kihemko nilionao, familia yangu na watoto wangu, uzoefu nilionao na watu ni mkubwa sana.

"Tuko katika mwelekeo sahihi na tumepiga hatua kubwa. Bado tuna mengi ya kufanya na nina hisi njaa kutoka kwa umiliki, bodi hadi kwa wachezaji na wafanyikazi wote hapa. Hili ndilo lengo letu, kufanya vizuri."



# Barcelona kumbakisha de Jong

**BARCELONA, Hispania**

MKURUGENZI wa michezo wa Barcelona, Deco amethibitisha kuwa klabu hiyo ina mpango wa kumbakisha kiungo Frenkie de Jong.

Hivi karibuni ripoti ilidai kuwa De Jong anaweza kufikiria mustakabali wake katika klabu hiyo mwishoni mwa msimu huu kwa sababu ya matatizo yake yanayoendelea na wasimamizi, ambayo yamechangiwa na kukataa kufanyiwa upasuaji wa jeraha la mguu ambalo limemfanya kuwa nje tangu Aprili.

Manchester United kwa mara nyingine wamehusishwa, lakini Deco alisisitiza kuwa Barcelona haitazamii kumuuza Mholanzi huyo.

"Sielewi mazungumzo yote kuhusu Frenkie," alisema Deco.

"Ana mkataba na Barca na tuna furaha naye sana. Ni mchezaji ambaye tunatamani kumuona akirejea kwa sababu tunamuhitaji Frenkie.

"Tunataka abaki, lakini mchezaji ataamua kwa wakati ufaao. Sio suala kwa sasa. Cha muhimu ni kwamba Frenkie anacheza nasi tena, kwa sababu tunamuhitaji na tunamthamini sana."

Aliyekuwa mgombea urais wa Barcelona, Victor Font hivi majuzi alidai kuzungumza na De Jong, akidai kusita kwa kiungo huyo kufanyiwa upasuaji wa mguu wake kunatokana na klabu hiyo kutokuwa na uwezo wa kuhakikisha kwamba utaratibu huo utafanya kazi.

Ripoti zinasema Barcelona imemuonya De Jong kwamba lazima ajitangaze kuwa yuko fiti hivi karibuni iwapo ataendelea kukataa kufanyiwa upasuaji, ingawa mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi anatarajiwa kusubiri hadi ajihisi yuko sawa kwa 100% kabla ya kurejea.

# Al Ahli yathibitisha ilimtaka Vinicius

**RIYADH, Saudi Arabia**

MKURUGENZI wa klabu ya Al Ahli ya Saudi Arabia amethibitisha kuwa klabu hiyo ilikuwa na mpango wa kumsajili winga wa Real Madrid Vinicius Junior katika majira haya joto.

Wafanyabiashara wa Saudia walimtambua Vinicius kama shabaha kubwa katika dirisha la usajili la majira ya kiangazi lakini walishindwa kumshawishi mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil kuhamia kwao.

Kulikuwa na ripoti za ofa ya rekodi ya dunia ya euro milioni 500 lakini 90min inaelewa kuwa hizo zimekataliwa na maofisa wa Saudi.

Al Ahli walimpoteza Allan Saint-Maximin aliyetimkia Fenerbahce na Mkurugenzi Khaled Al Issa alithibitisha awali walikuwa na mpango wa kumnunua Vinicius kabla ya hali ambayo haikutarajiwa kuwafanya kubadili mtazamo wao kwa mshambuliaji huyo, na kumsajili Ivan Toney kutoka Brentford.

"Kamati yenye uwezo wa kiufundi, ambayo ni pamoja na Mkurugenzi wa ufundi, iliamua kumruhusu Saint-Maximin kuondoka kwa sababu ilikuwa rahisi katika suala la mchakato wa mauzo, na kiasi cha mkataba kinaweza kubebwa na klabu nyingine yoyote," alisema Al Issa akiiambia Kora Rotana. .

"Kulikuwa na nia ya kumleta winga mkubwa sana Vinicius kutoka Real Madrid, lakini wakati wa mazungumzo kitu ambacho hakikutarajiwa kilitokea na mpango huo kufa.

"Kipaumbele chetu kilihama kutoka kwa winga hadi mshambuliaji kulingana na kuondoka kwa Al Buraikan, na tuliingia kwenye mazungumzo na Ivan Toney na Victor Osimhen, na yalimalizika kwa kuwasili kwa Toney."

Hakuna winga mbadala aliyesajiliwa kabla ya dirisha la usajili kufungwa na Al Issa aliapa kufanya usajili wa maana haraka iwezekanavyo, ingawa alisita kusema kwamba kunaweza kuwa na uhamisho mwingine wa Vinicius.

"Firas Al Buraikan hakuingia kwenye mpango wa ufadhili wa masomo na kwa hivyo aliendelea na sisi," Al Issa alielezea. "Kutokana na hilo, pengo lilitokea katika nafasi ya mrengo, na tutafanya kazi kuimarisha nafasi hii kwa makubaliano ambayo yanazidi matarajio ya mashabiki wa Al Ahli wakati wa majira ya baridi."

HABARI MICHEZO

# KANU AELEZEA MACHUNGU KATIKA SAFARI YAKE YA SOKA

**Na Christina Mwakangale**

NGULI wa soka Barani Afrika kutoka Nigeria aliyewahi kuzichezea klabu mbalimbali Ulaya, Nwankwo Kanu amesema akiwa mchezaji anakumbuka wakati mgumu aliopitia alipougua ugonjwa wa moyo na kulazimika kukaa nje kwa takribani mwaka mmoja.

Kanu, ambaye pia ni Mwanzilishi na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Kanu Haert Foundation, amesema kutokana na kuwa miongoni mwa wenye tatizo hilo alianzisha taasisi hiyo nchini Nigeria ili kufanikisha huduma hasa upasuaji wa moyo.

Kanu, alisema hayo jana baada ya kutembelea wagonjwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)-Mloganzila, Dar es Salaam, wakiwamo watoto wenye maradhi ya moyo.

"Taasisi yangu nilianzisha mwaka 2000 na tayari watoto 690 wa Afrika wamefanyiwa upasuaji wa moyo wa kufungua kifua, ingawa upasuaji huu mara nyingi unafanyika nje ya nchi, hasa Israel, India na Uingereza," alisema Kanu.

Alisema upasuaji huo kufanyika nje ya Nigeria ni ghali kutokana na watoto kuambatana na mzazi na huduma ya matibabu aina hiyo huwapasa kukaa nje kwa siku nyingi.

"Nimefika kwa sababu mimi ni kama nembo kwa wagonjwa hawa. Nakumbuka nikiwa mchezaji tatizo langu kubwa lilikuwa moyo, nilifanyiwa upasuaji Ohio huko Marekani. Nilikaa nje kwa mwaka mmoja,nilikuwa na hofu ya kutocheza tena soka, lakini nililirejea uwanjani nikiwa na nguvu na hata kushinda tuzo mbalimbali.

"Kuja hapa leo ni furaha kwangu. Ninawapongeza madaktari wote na kuwaombea wagonjwa, watambue kwamba wanaposikia Kanu, wajue kwamba nami nilipitia changamoto hiyo lakini nilisimamaimara," alisema Kanu.



Kaimu Mkurugenzi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)-Mloganzila, Dk. Godlove Mfuko (kushoto), akizungumza na Mwanasoka wa zamani ambaye ni Mwanzilishi na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Kanu Heart Foundation, Nwanko Kanu (katikati) baada ya kutembelea hospitali hiyo kuwaona wagonjwa wakiwamo watoto wenye matatizo ya moyo. Kulia ni Mkurugenzi wa Mahusiano wa Vodacom Foundation, Zuweina Farah. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Mwandishi Nipashe achaguliwa Mwenyekiti Soka la wanawake

**Na Shufaa Lyimo**

MWANDISHI Mwandamizi wa Michezo kwenye gazeti la Nipashe, Somoe Ng'itu amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Soka cha Wanawake Tanzania (TWFA) katika uchaguzi uliofanyika jana Moshi Mkoani Kilimanjaro.

Mbali na Somoe, mwanahabari mwingine mwandamizi, Zena Chande wa gazeti HabariLEO alichaguliwa kuwa Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF).

Somoe alipata kura 37 na mpinzani wake Amina Karuma alipata kura 14, Zena alipata kura 34 na wapinzani wake Fatuma Seleman alipata kura tisa na Veronica Samo alipata kura nane.

Katika nafasi ya wajumbe wa Kamati ya utendaji, Irene Ishengoma, Ndinagwe Sungura walipita bila kupingwa baada ya Mwanaheri Kalolo kujitoa siku ya uchaguzi.

Baada ya Somoe kutangazwa na kuapishwa, alimteua Beatrice Mgaya kuwa Makamu Mwenyekiti na Hamisa Katambi kuwa mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya TWFA.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi huo, Benjamin Kalume baada ya kutangaza matokeo aliwataka viongozi hao wakafanye kazi kwa ushirikiano na kuvunja kambi kwani uchaguzi umemalizika.

## Yanga yatanguliza mguu mmoja

INATOKA UK. 24

kuanza kufokea mabeki wake kwa uzembe.

Ilikuwa ni zamu ya wenyeji kukosa bao dakika ya 30, baada ya kufanya shambulizi kali lililomkuta Omari Bashiru, ambaye shuti lake lilipaa juu ya lango.

Akiwa amebaki yeye na kipa, Dube kwa mara nyingine alikosa bao dakika ya 40 na kumkasirisha kocha Gamondi ambaye alionekana kufoka na kurusha mikono juu kwa hasira.

Shambulizi hilo lilianza kwa mpira uliorudishwa kimakosa na mmoja wa mabeki wa CBE na kumkuta Dube akiwa hajakabwa, akavuta hatua mbili na kumchagua kipa, akiwa hatua takriban sita tu kutoka langoni, mpira wake ukatoka nje.

Baada ya kosakosa nyingi, hatimaye Dube alisawazisha makosa yake alipoukwamisha mpira wavuni sekunde chache kabla ya mapumziko, alipomalizia vizuri pasi kutoka kwa Stephane Aziz Ki.

Kipindi cha pili kwa nyakati tofauti Yanga ilifanya mabadiliko, mwanzoni kabisa ikiwatoa Aziz Ki na Dube na nafasi zao kuchukuliwa na Clatous Chama na Clement Mzize, baadaye wakaingia tena Yao Koassi na Duke Abuya kuchukua nafasi za Mudathir Yahaya na Maxi Nzengeli, na dakika tano kabla ya mechi kumalizika aliingia Jean Baleke akipishana na Pacome.

Kabla ya kutoka, Mudathir nusura afunge bao dakika ya 70 baada ya shuti lake kali kuwababatiza mabeki na mpira ukarejea kwa Boka ambaye alipiga krosi iliyounganishwa vibaya na Mzize, ukatoka nje.

Mzize akiwa hatua mnne tu kutoka langoni, alipaisha mpira akiwa peke yake dakika ya 42, baada ya makosa ya walinzi wa CBE waliompa muda wa kuuweka kifuani na kugeuka.

Ilikuwa ni rahisi zaidi kupata bao kuliko kukosa kama alivyofanya Chama dakika za majeruhi, alipowekewa krosi nzuri na Mzize lakini akiwa kwenye nafasi ya kufunga aliunganisha kwa mguu wa kushoto mpira ulionda nje kidogo ya goli.

Yanga inarejea nchini leo kuwasubiri Waethiopia kwa ajili ya mchezo wa marudiano.

## Che Malone: Tutawashangaza Al Ahly

INATOKA UK. 24

na nadhani kila kitu kitaenda kama kilivyopangwa," alisema.

Mchezo huo unatarajiwa kuanza majira ya saa 2:00 usiku kwa saa za Afrika Mashariki na timu hizo zitarudiana wiki ijayo jijini Dar es salaam.

Huu utakuwa mchezo wa kwanza wa kimataifa msimu huu kwa Simba, kwani haikucheza mechi yoyote hatua ya awali kutokana kuwa kwenye kiwango cha juu ndani ya 10 bora Afrika, ambapo imekuwa na faida ya kutocheza michezo ya awali, badala yake kwenda moja kwa moja raundi ya kwanza.

# Michezo

Jumapili Septemba 15, 2024

Nipashe





Wakala afichua Nico Williams hakutaka kuihama klabu yake UKURASA 21

## Che Malone: Tutawashangaza Al Ahly Tripoli

**Na Adam Fungamwango**

BEKI kisiki wa Simba, Che Fondoh Malone, amesema yeye na wachezaji wenzake wapo tayari kwa mchezo wa leo wa raundi ya kwanza, Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Al Ahly Tripoli ya Libya na watawashangaza wapinzani wao hao.

Akizungumza kutoka nchini humo ambako mchezo wa mkondo wa kwanza utachezwa kwenye uwanja wa Juni 11, jijini Tripoli, Che Malone amesema wanataka kushinda si mchezo wa kesho tu, bali yote ambayo timu yao itakabiliana nayo katika mechi za Kombe la Shirikisho.

"Mimi niko tayari na hata wenzangu wapo tayari, kwa mechi ya ya kesho (leo), najua haitokuwa rahisi, ni kweli hii si Ligi ya Mabingwa, ni Kombe la Shirikisho, lakini huwezi kudharau kwa sababu mara nyingi ni timu zile zile za kiwango kile kile zinazocheza michuano yote miwili kila msimu, tutawashangaza wapinzani wetu, tumekuja kupambana kupata ushindi," alisema Che Malone.

Alisema maandalizi ya mchezo huo hayakuanza hivi karibuni, au kwenye mapumziko ya kalenda za FIFA, bali mwanzoni mwa msimu.

"Maandalizi yamekamilika kwa sababu yalianza zamani, hayajaanza sasa, siwezi kusema eti yamefanyika kipindi cha mapumziko ya FIFA hapana, yalianza kabla ya msimu.

Malengo ya klabu yameshawekwa wazi, hivyo sisi wachezaji tunachofanya ni kuyafanyia kazi, tulicheza mechi ya kirafiki dhidi ya Al Hilal ya Sudan timu ambayo mara nyingi inafuzu hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika na wakati mwingine inacheza nusu fainali, kilikua kipimo tosha kwa sababu wachezaji wengine ambao hawakuwahi kucheza michuano ya CAF, ilikuwa ni nafasi nzuri ya kujionea mambo yanavyokuwa," alisema.

Alisema pamoja na kwamba Simba ina rekodi nzuri ya michezo ya kimataifa, lakini wao hawaangalii hilo, badala yake watalazimika kupambana ili kutimiza malengo.

"Tunahitajika kupambana na kushinda kila mechi inayokuja kwa sababu kufuzu michuano ya CAF siyo jambo rahisi, tunakwenda kucheza mechi na kushinda kwa ajili ya kupambania kombe, tunajiamini

INAENDELEA UK 23



Mshambuliaji wa Yanga, Prince Dube (kulia) akiwatoka wachezaji wa CBE ya Ethiopia kwenye mchezo wa kwanza hatua ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika jana, mchezo huo ulichezwa Addis Ababa na Yanga kuibuka na ushindi wa bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA YATANGULIZA MGUU MMOJA MAKUNDI CAF

## ●●● Ni baada ya kuibuka na ushindi mbele ya CBE, lakini kocha Gamondi......

**Na Adam Fungamwango**

BAO pekee lililofungwa na straika raia wa Zimbabwe, Prince Dube, limeiweka Yanga katika mazingira mazuri ya kutinga hatua ya makundi, Ligi ya Mabingwa Afrika, ushindi wa 1-0 dhidi ya mwenyeji CBE ya nchini Ethiopia.

Hata hivyo, licha ya Yanga kuibuka na ushindi huo, Kocha wao Miguel Gamondi ameonesha kutofurahishwa na safu yake ya ushambuliaji kukosa magoli mengi kwenye mchezo huo.

Baada ya mchezo Gamondi alisema walistahili kuondoka na ushindi wa idadi goli zaidi ya moja lakini hawakufanikiwa kutokana na kupoteza nafasi nyingi za wazi.

"Nimefurahi tumepata ushindi, lakini sijaridhishwa na namna tulivyopoteza nafasi nyingi, tulistahili ushindi mkubwa zaidi, tutalifanyia kazi suala hili," alisema Gamondi.

Maxi Nzengeli

Katika mchezo huo wa jana mkondo wa kwanza, hatua ya kwanza ya ligi hiyo uliochezwa saa 9:00 alasiri kwa saa za Tanzania, Uwanja wa Abebe Bikila, jijini Addis Ababa, Yanga ingeweza kuibuka na ushindi wa mabao mengi kutokana na wachezaji wake, hasa Dube kukosa mabao kadha ya wazi katika namna iliyowaacha midomo wazi mashabiki wengi.

Kwa ushindi huo, Yanga inatakiwa kupata ushindi au sare yoyote nyumbani, Septemba 20, Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar, ili itinge hatua ya makundi kwa mara ya pili mfululizo kama ilivyofanya msimu uliopita.

Dakika ya pili tu Yanga walianza kubisha hodi langoni mwa wenyeji wao, na Dube alikosa bao lililookolewa na kipa Firew Getahun Alemayehu.

Dakika moja baadaye CBE ilijibu shambulizi hilo kupitia kwa mchezaji wake Adis Gebal, ambaye aliwatoka walinzi wa Yanga na kuachia shuti lililowababatiza mabeki, mpira ukarudi na kumkuta Fuad Abdul ambaye alipiga shuti lingine lililodakwa vyema na kipa Djigui Diarra.

Dube aliendelea kukosa mabao, kwani dakika ya 12, aliunganisha kwa mguu wa kushoto krosi iliyotoka kwa Pacome Zouzoua, na mpira ulionekana kama unaingia wavuni, lakini kwa mshangao wa wengi uligonga nguzo ya pembeni na kurejea uwanjani, kabla ya mabeki wa CBE kuuondosha kwenye hatari.

Dakika sita baadaye nusura Yanga iandike bao, baada ya mpira wa kona uliookolewa na mabeki kumkuta Pacome akiwa kwenye eneo zuri, aliachia mkwaju mkali wa chinichini ambao ulitoka nje kidogo ya lango na kumfanya kipa, Alemayehu,

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >